# Maono

## Ya Mheshimiwa Rais

TOLEO LA KWANZA: Siku 100 za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Machi, 2026



#KaziNaUtuTunasongaMbele

# WADHAMINI



**Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba**
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



**Mhe. Hamza S. Johari**
Mwanasheria Mkuu wa Serikali



**Bw. Nehemiah Kyando Mchechu**
Msajili wa Hazina




**Mhe. Paul Christian Makonda**
Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo



**Mhe. Deogratius John Ndejembi**
Waziri wa Nishati



**Mhe. Abdallah Hamis Ulega**
Waziri wa Ujenzi



**Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo**
Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi



**Dkt. Juma Zuberi Homera**
Waziri wa Katiba na Sheria



**Jeremiah Yoram Katungu**
Kamishina Jenerali wa Magereza



**Bw. Masha J. Mshomba**
Mkurugenzi Mkuu wa NSSF



**Eng. Hassan Seif Saidy**
Mkurugenzi Mkuu wa REA



**Bw. Lazaro Twange**
Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO



**CPA(T) Mussa Makame**
Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC



**Eng. Charles Sangweni**
Mkurugenzi Mkuu wa PURA



**Dr. Baghayo Abdallah Saqware**
Kamishna wa Bima TIRA



**Eng. Victor H. Seff**
Mtendaji Mkuu wa TARURA



**Bw. Samuel A. Mshote**
Mkurugenzi Mkuu wa TFC

**MWEZESHAJI**



**Bi. Asha Dachi**
Mkurugenzi Mtendaji wa TSN



# Mwelekeo wa Serikali ya Rais Samia kujenga Taifa jumuishi, linalojitegemea

Na Anastazia Anyimike

SERIKALI ya Awamu ya Sita kipindi cha pili chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imeweka bayana mwelekeo wake wa kuendeleza ukuaji wa uchumi kwa manufaa ya Watanzania wote ikienda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050).

Dhamira kuu ni kujenga taifa jumuishi, lenye ustawi, haki na linalojitegemea kiuchumi.

Katika mkakati huo, serikali imelenga kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kutoka asilimia 5.6 ya sasa hadi zaidi ya asilimia saba ifikapo mwaka 2030, hatua itakayoboresha huduma za kijamii na kuimarishwa kwa miundombinu wezeshi ya kiuchumi na kuimarisha ustawi wa wananchi.

Katika kufikia azma hiyo, serikali imeweka mikakati ya kuwekeza zaidi kwenye sekta zinazoajiri watu wengi zikiwamo kilimo, utalii, viwanda, ujenzi na madini.

Akizindua Bunge la 13 Novemba mwaka jana jijini Dodoma, Rais Samia anasema mwelekeo wa serikali ni kukua kwa pamoja kwa uchumi unaogusa maisha ya mtu mmoja mmoja na uchumi jumla.

Anasema katika kufikia azma hiyo, serikali itaimarisha masoko ya mitaji kwa kuhamasisha uwekezaji wa ndani, pamoja na kutumia rasilimali kama madini kudhamini mikopo ya uwekezaji badala ya kuweka mzigo mkubwa kwenye Deni la Taifa.

Rais Samia anasema kwa kutambua kuwa sekta binafsi hasa za ndani ni nguzo muhimu katika ukuzaji wa uchumi, serikali itaboresha zaidi mazingira ya biashara kwa kukamilisha utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI) na mapendekezo ya Tume ya Kuboresha Mifumo ya Kodi.




Pia itaweka nguvu kudhibiti mfumuko wa bei, kutoa motisha kwa viwanda vya ndani, kuongeza vivutio vya kikodi na visivyo vya uwekezaji kwa vijana.

Rais Samia anasema mwelekeo wa serikali ni kuwa na wawekezaji vijana ifikapo mwaka 2030 watakaozalisha ajira za wenzao ili kufikia lengo la serikali za kuzalisha ajira milioni 8.5 katika sekta mbalimbali.

Anasema katika kufikisha hilo, serikali itahamasisha vijana na wamiliki wa biashara ndogo kupata elimu ya biashara na kujisajili katika mfumo wa manunuzi wa serikali na kuja na programu maalumu za mafunzo ya ufundi zitakazounganishwa na miradi mikubwa ya kimkakati kama Reli ya Kisasa (SGR), bandari, uchumi wa buluu, madini na gesi na kuboresha mikopo ya asilimia 10.

## Uwezeshaji wa wanawake na wafanyabiashara wadogo

Aidha, Rais Samia anasema kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wa maendeleo, serikali itahamasisha ufadhili wa biashara za wanawake wanaofanya kazi kwenye masoko na kuratibu mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili wakopesheke.

Pia itaboresha miundombinu ya masoko, mifumo wa majisafi na majitaka, huduma za afya na vituo vya kutunza watoto kwenye masoko ili wafanyabiashara wanawake wafanye shughuli zao katika mazingira salama na yenye tija.

Anasema serikali pia italipa kipaumbele suala la utengaji wa maeneo ya biashara kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati ili kuwarasimisha na kuwaingiza kikamilifu katika mfumo rasmi wa uchumi.

## Huduma za kijamii

Rais Samia anasema serikali imejipanga kufikia asilimia 100 ya upatikanaji wa majisafi, salama na ya uhakika na kuongeza nguvu ya kuyafikia maeneo ambayo upatikanaji wa maji bado ni changamoto.


Pia inakwenda kukamilisha ujenzi wa Gridi ya Taifa ya Maji na kuendelea na ukamilishaji wa miradi ya maji na ujenzi wa mabwawa makubwa ya maji.

Kwa upande wa sekta ya afya, Rais Samia anasema mbali na Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, mwelekeo ni kuwekeza zaidi katika kinga, kuongeza ajira za watumishi wa afya na kukamilisha hospitali, vituo vya afya na zahanati.

Serikali pia itaendelea kuboresha huduma za kibingwa na uwezo wa vitanda katika Hospitali ya Taifa Muhimbili ili iwe tumaini la nchi za Afrika Mashariki, sambamba na








kuimarisha huduma za kibingwa katika hospitali za rufaa za mikoa na kanda zitaongezewa uwezo ili kupunguza rufaa nje ya mikoa.

Anasema serikali pia itajielekeza katika kuongeza uwezo wa uzalishaji wa dawa na vifaatiba, na vitendanishi ili kupunguza utegemezi wa kuagiza nje na utafiti wa dawa asili.

Katika elimu, anasema mkazo utawekwa kwenye masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM), kuongeza mikopo ya elimu ya juu na kuhakikisha kila wilaya ina chuo cha ufundi stadi (VETA) chenye vifaa vya kisasa.

Pia miundombinu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu nayo itapewa kipaumbele ili kutekeleza programu ya elimu jumuishi.

## Sekta za uzalishaji

Rais Samia anasema serikali imejipanga kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta ya kilimo kutoka asilimia nne hadi 10 ifikapo mwaka 2030 kwa kuimarisha kilimo cha umwagiliaji kwa kuongeza ekari milioni tano kutoka ekari milioni 3.4 za sasa.

Pia kuongeza matumizi ya pembejeo na teknolojia kwa kuanzisha vituo vya ukodeshaji zana za kilimo za kisasa.

Rais Samia anasema serikali pia imekusudia kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa mahindi, mchele, mbogamboga barani Afrika na kuongeza uzalishaji wa sukari na mafuta ya kula.

Pia ikisimamia kwa karibu mazao ya kimkakati kama chai, kahawa, parachichi na pamba yakisimamiwa kwa karibu zaidi.

Katika sekta ya ufugaji, anasema lengo ni kuongeza maeneo yaliyopimwa kwa ufugaji hadi ekari milioni sita kutoka ekari milioni 3.5, kuboresha chanjo na utambuzi wa mifugo na kosafu za mifugo katika kuyafikia masoko ya kimataifa.

Kwa upande wa uvuvi, serikali italipa kipaumbele suala la maendeleo ya uchumi wa buluu, sekta ya uvuvi na kilimo cha kisasa cha mazao ya baharini.

Itakamilisha bandari ya kisasa ya uvuvi ya Kilwa na kujenga ya Bagamoyo itakayofungamanishwa na kongani ya viwanda vya samaki na kuendelea na utoaji wa mikopo kwa wavuvi.

Katika viwanda, Rais Samia anasema mwelekeo ni kuongeza ukuaji wa sekta hadi asilimia 9 kutoka asilimia 4.8 ifikapo 2030.

Pia kulifanya taifa linalojitegemea kwa kuwa na viwanda vitakavyolisha viwanda vingine kwa malighafi na vipuri na vinavyozalisha bidhaa zinazohitajika kwenye masoko ya kikanda.

Rais Samia anasema pia kongani za viwanda zitaanzishwa katika kila wilaya ili kuongeza thamani ya mazao na madini.

## Sekta ya madini

Rais Samia anasema mkakati wa serikali ni kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara ya madini yote Afrika Mashariki na Kati ifikapo mwaka 2030 na kuongeza umakini katika kusimamia uwekezaji wa madini ya kimkakati.

Pia kutenga maeneo maalumu kwa wachimbaji wadogo na kuwapatia mitaji na mitambo ya uchorongaji na kuendelea kununua dhahabu ili kuimarisha soko na kupunguza utoroshaji wa madini, na serikali itaanzisha Mfuko wa Wakfu wa Madini kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Rais Samia anasema serikali imelenga kufikia watalii wa ndani na nje milioni nane ifikapo mwaka 2030 kwa kuboresha vivutio na kuunganisha bidhaa za utalii ili kuongeza muda wa kukaa kwa watalii.

## Sekta wezeshi

Serikali imebainisha itaendelea kuimarisha miundombinu wezeshi ya umeme, bandari, reli na barabara.

Rais Samia anasema kwa sekta ya nishati, serikali imelenga kuzalisha megawati 8,000 ifikapo 2030, kupanua Gridi ya Taifa ya Umeme na kuimarisha usalama wa mafuta.

Pia inaweka kupaumbele cha kutekeleza mkakati wa nishati safi ya kupikia ili ufikie asilimia 80 ya watumiaji ifikapo mwaka 2034.

Anasema serikali itaendelea kuwekeza katika SGR, barabara, madaraja, bandari na viwanja vya ndege ili kujenga mfumo fungamanishi wa usafiri na usafirishaji.

Pia maboresho ya bandari na kuimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania ni sehemu ya mkakati wa kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utalii, biashara na usafiri kikanda.

## Sekta ya TEHAMA

Rais Samia anasema serikali itaongeza uwekezaji katika TEHAMA ili mifumo ya serikali isomane na kuboresha utoaji huduma, sambamba na kujenga Chuo cha Teknolojia ya Kidijitali ili kuwajengea vijana uwezo wa kushindana kimataifa.

## Utamaduni na Michezo

Anasema serikali itaendeleza Kiswahili kama bidhaa ya kimataifa, kukuza sanaa, filamu na muziki, na kuwekeza katika michezo kama sekta ya kiuchumi ikiwamo maandalizi ya mashindano ya AFCON 2027.

## Utawala bora na ushirikiano wa kimataifa

Rais Samia anasema serikali itaendelea kupambana na rushwa, kuboresha utumishi wa umma na kuimarisha mashirika ya umma ili yawe na tija.


Pia ushirikiano na Mahakama utaimarishwa kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati pamoja na kutafsiri sheria kwa Lugha ya Kiswahili.

Kwa upande wa sera ya nje, anasema Tanzania itaendelea kufuata misingi ya kutofungamana na upande wowote, kupanua fursa za kiuchumi na kulinda heshima na uhuru wa taifa.

Anasema pia vyombo vya ulinzi na usalama vitaimarishwa ili kulinda mipaka ya nchi, raia na mali zao.

Kwa ujumla, mwelekeo wa Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kujenga uchumi shindani, jumuishi na unaojitegemea.

Rais Samia anasema mwisho wa Awamu ya Sita hautapimwa tu kwa miradi mikubwa ya maendeleo, bali pia kwa tabasamu la utu na ustawi litakaloonekana katika maisha ya Watanzania.





Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu Na Wenye Ulemavu)

# MAFANIKIO YA SIKU 100 BAADA YA SERIKALI KUINGIA MADARAKANI

## UTANGULIZI

RAIS Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa ahadi mbalimbali kwa wananchi wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu zilizofanyika Agosti hadi Oktoba, 2025. Ametoa ahadi za siku 100 baada ya kuchaguliwa Oktoba 29, 2025 na kuingia madarakani Novemba 03, 2025 akianza kuongoza kipindi cha pili cha awamu ya sita. Pia wakati akifungua Bunge la 13 Novemba 14, 2025 amesisitiza kuanza utekelezaji wa ahadi hizo.

Baada ya kuunda serikali, Rais Samia ameanza utekelezaji wa ahadi katika sekta za afya, elimu, maji, kurasimisha sekta isiyo rasmi, kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya wafanyabiashara ndogo, za kati na uendeshaji wa kampuni changa.

Rais aliahidi kuunda Tume ya Kuanzisha Mazungumzo ya Maridhiano na Upatanishi pamoja na kuandaa mazingira ya kuanza kwa mchakato wa mabadiliko ya Katiba. Utekelezaji wake, imeundwa Tume Huru ya Uchunguzi wa matukio ya uvunjifu wa amani yaliyotokea wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Matokeo ya uchunguzi huo yatawezesha kuanzisha mazungumzo ya maridhiano na upatanishi na kuanza kwa mchakato wa mabadiliko ya Katiba.

SEKTA ya Fedha imeongeza mapato yaliyokusanywa na TRA, kati ya Novemba na Desemba, 2025 zilikusanywa Sh trilioni 6.99 na hivyo kuvuka lengo la kukusanya Sh trilioni 6.86 sawa na asilimia 101.89.

Imedhibiti mfumuko wa bei ndani ya viwango vinavyokubalika ambapo Novemba 2025, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.4 na Desemba 2025 ulifikia asilimia 3.6. Viwango hivyo, vipo ndani ya lengo la nchi la muda wa kati la asilimia 3.0 hadi 5.0, ndani ya vigezo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) usiozidi asilimia 8.0 na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ya wigo wa asilimia 3.0 hadi 7.0.

Imeimarisha akiba ya fedha za kigeni na kufikia dola za Marekani milioni 6,329 Desemba, 2025, kiwango ambacho kinatosha kugharamia mahitaji ya miezi 4.9 ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje. Kiwango hicho kimezidi vigezo vya kitaifa vya kuanzia miezi minne na vile vya EAC vya kuanzia miezi 4.5.

Imepunguza nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nje ya nchi kufikia dola za Marekani milioni 609.7 Desemba, 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 657.5 katika kipindi cha 2024.

Imeongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi kufikia dola za Marekani milioni 10,002.8 kuishia Desemba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 9,376.6 mwaka 2024.

SEKTA ya Mipango, imefanikiwa kuandaa Mpango Elekezi wa Muda Mrefu 2050 (LTPP 2050) ambao ni nyenzo ya kimkakati ya utekelezaji wa Dira 2050 yenye lengo la kuiwezesha Tanzania kufikia hadhi ya nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu, ikiwa na pato la Taifa la dola za Marekani trilioni moja, na wastani wa pato la mtu la dola za Marekani 7,000 kwa mwaka.

Pia imeandaa Mpango wa Pili wa Maboresho ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI II) kwa kuzingatia maono ya Dira 2050. Mpango huo unalenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

SEKTA ya Uwekezaji imeanzisha Kituo Maalum cha kuhudumia na kuwezesha wawekezaji vijana kilichopo Mabibo - Dar es salaam kitakachotoa huduma za mafunzo, uwezeshaji na usaidizi kwa wawekezaji vijana.

Pia imeanzisha programu maalum ya kuwezesha wawekezaji vijana kubuni na kuanzisha viwanda mkoani Dodoma (Nala, ekari 100), Pwani (Kwala, ekari 20 na Bagamoyo, ekari 20), Mara (Bunda, ekari 100) na Ruvuma (Songea, ekari 100).

SEKTA ya Afya imepata mafanikio ya kuanza kutumika kwa huduma ya Bima ya Afya kwa Wote kwa awamu ya kwanza ya wananchi wasio na uwezo watakaogharamiwa na Serikali tangu Januari 26, 2026.

Pia imetoa Sh bilioni 48.78 kwa ajili ya kuanza kugharamia Bima ya Afya kwa wote kwa awamu ya kwanza kwa wananchi 1,457,602 sawa na kaya 276,004 zisizo na uwezo, wazee 235 na watoto 265 wanaoishi kwenye makazi yanayomilikiwa na Serikali.

Pia imekamilisha Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano wa Bima ya Afya kwa wote (2025/26-2030/31) unaolenga kuwaelimisha wananchi ili waone umuhimu wa kujiunga na Bima ya Afya.

Vile vile, imeanza kugharamia magonjwa





sugu ya saratani, figo, moyo, kisukari na mifupa kwa wananchi wasio na uwezo kupitia mfuko wa kugharamia bima ya afya. Katika awamu ya kwanza zimetumika Sh bilioni 6.8 kugharamia matibabu ya magonjwa sugu na huduma za dharura.

Pia imefufua kiwanda cha Tanzania Pharmaceutical Industries (TPI) cha kuzalisha dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI (ARVs), kwa kushirikiana na sekta binafsi ambapo Serikali inamiliki asilimia 70 ya hisa. Kiwanda kinatarajiwa kuanza uzalishaji Juni, 2026.

Pia imeondoa zuio la kuchukua miili ya marehemu katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya kote nchini kwa kigezo cha kutokulipia gharama za matibabu na madeni.

Pia imetoa Sh bilioni 39.3 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za uzazi na watoto wachanga kwenye vituo vya kutolea huduma za afya 89 ikijumuisha hospitali za wilaya 20, vituo vya afya 19 na zahanati 50.

Imeongeza idadi ya vituo vya kutoa huduma za upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni kutoka 523 Oktoba 2025 hadi 578 Januari 2026, hivyo idadi ya wanawake kujifungulia vituoni imeongezeka kutoka asilimia 85 Oktoba, 2025 hadi 87.5 Januari 2026.

SEKTA ya Elimu imepata mafanikio katika elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu kwa kukamilisha ununuzi na usambazaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya Sh bilioni 5.4 kwa walimu na wanafunzi wenye mahitaji maalum. Pia imechapa na kusambaza vitabu milioni 18 vya ziada ili kuboresha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi na ujifunzaji.

Pia imezindua na kuanza utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu wenye kaulimbiu: 'Mtoto Asome, Aandike na Ahesabu bila shida' unaolenga kuongeza ubora wa elimu ya msingi na mbinu bora za kufundishia.

Pia imetoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 600 wa sekondari na wasimamizi 604 ngazi ya mkoa na halmashauri. Pia imesambaza vifaa vya TEHAMA katika shule 600 za msingi na 422 za sekondari ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia teknolojia hiyo.

Pia inaendelea na ujenzi wa vyuo vya VETA 64 katika wilaya nchini na umefikia wastani wa asilimia 67 na cha mkoa wa Songwe kimefikia asilimia 68.

Pia imefungamanisha mifumo ya teknolojia ya elimu, kwa kuunganisha Mfumo wa Usimamizi wa Kujifunza (LMS) wa elimu ya sekondari, TET- Soma Kwanza TV, na madarasa janja yaliyopo Dar es Salaam, Pwani na shule ya msingi Mtakuja Zanzibar na sekondari ya Dkt. Samia Dodoma kwa lengo la kuongeza matumizi ya teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji.

Pia imeimarisha ubora wa elimu ya juu kwa kutoa mikopo ya Sh bilioni 348.77 kwa wanafunzi 107,541 wa mwaka wa kwanza, kati yao wa shahada ya kwanza ni 94,451, shahada za juu 310 na diploma 11,844.

Vilevile imetoa mikopo ya Sh bilioni 550.44 kwa wanafunzi 177,492 wanaoendelea na masomo wakiwemo wa shahada ya kwanza 170,413, shahada za juu 108 na diploma 6,053.

Imetoa ufadhili wa Sh bilioni 10.5 kupitia SAMIA Scholarship kwa wanafunzi 1,786 wanaosoma sayansi katika vyuo bora duniani. Pia imetoa ufadhili wa Sh bilioni 5.487 kupitia SAMIA Extended DS/AI+ wa kusoma shahada ya kwanza kwa wanafunzi 50 wenye ufaulu wa juu kidato cha sita katika tahasusi za (PCM, PGM na PMC) ambao walichaguliwa kusoma fani za sayansi data, akili unde na sayansi shirikishi.

Imekamilisha Mkakati wa Usawa wa Kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu wa 2025/26- 2029/30 wenye lengo la kuimarisha mifumo na miundombinu itakayowezesha ufikiaji wa usawa wa kijinsia na elimu jumuishi katika taasisi za elimu ya juu.

SEKTA ya sayansi, teknolojia na ubunifu imefanikiwa kupata mikopo ya Sh milioni 667 katika awamu ya kwanza kwa wabunifu saba kupitia Mfuko wa "Samia Commercialization Fund" ili kuwezesha ubiasharishaji wa bunifu na teknolojia zao na kukamilisha.

Pia imeidhinisha mkakati wa kitaifa wa kuhamasisha mchango wa diaspora katika shughuli za elimu, sayansi, teknolojia na ubunifu.

SEKTA ya Maji inakamilisha miradi 16 Dodoma, Njombe, Iringa, Kilimanjaro, Geita, na Tanga kwa Sh bilioni 16.28 na kunufaisha zaidi ya wananchi 118,400.

Inaeendelea na ujenzi wa miradi ya maji 71 inayotekelezwa nchini ukiwemo wa Mtwara, Tanga, Dodoma, Tabora na Dar es Salaam kwa Sh bilioni 142.8 ambayo itanufaisha wananchi 2,887,029.

Imelipa Sh bilioni 198.84 kwa wakandarasi na wataalamu washauri wa miradi mbalimbali ikiwemo wa bwawa la Kidunda. Pia fidia ya Sh bilioni 4.8 kwa wananchi 210 wa Morogoro, Babati, Makambako na Tanga.

Vile vile, imesaini mikataba ya utekelezaji wa miradi ya maji Morogoro wa Sh bilioni 81.4 utakaonufaisha wananchi 602,000 na wa

kusafirisha majitaka Mwanza wa Sh bilioni 38.7 na utakaonufaisha kaya 3,400. Pia imesaini mkataba wa miradi mitano wa Sh bilioni 2.66 utakaotekelezwa Mbeya, Njombe, Geita, Singida na kunufaisha wananchi 186,580.

Pia inakamilisha ununuzi na ufungaji wa dira za maji 2,271 za malipo ya kabla.

Vile vile, inaendelea na ujenzi wa mabwawa matatu ya kuvuna maji ya mvua Gidahababieg (Hanang), Mwambazi (Sumbawanga) na Mwamashindike (Maswa) yenye ujazo wa mita za ujazo 1,457,000 utakaonufaisha wananchi 1,817,800 na mifugo 356,400.

Pia inaendelea na utekelezaji wa miradi ya dhana ya Mtandao wa Taifa wa Kusambaza Maji kwa kuanza utekelezaji wa miradi wa kukamilisha usanifu wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Dodoma kupitia Singida (LVD).

SEKTA ya Kilimo nchini imefanikiwa kusambaza mbolea ya ruzuku tani 319,632 ya Sh 512,465,277,981 kwa wakulima 532,023 na taasisi 777 Tanzania Bara. Kati ya gharama hizo, Sh 384,223,259,670 ni mchango wa wakulima na Sh 128,242,018,312 ni ruzuku ya Serikali.

Kusambaza viuatilifu vya Sulphur ya unga tani 44,177.18 na ya maji lita 2,142,874.50 vya Sh 218,781,054,320 kwa wakulima wa korosho kwa mpango wa ruzuku katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Tanga na Pwani.

Kuzalisha na kusambaza tani 37,557.18 za mbegu bora kwa mfumo wa ruzuku kwa wakulima wa mahindi, alizeti na korosho.

Imesajili na kurasimisha wakulima 532,023 kwenye mfumo rasmi wa mbolea ya ruzuku. Imenunua unit 1,200 za pampu, jenereta na mipira kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima Tanzania bara ambazo zitaongeza eneo la umwagiliaji kwa ekari 48,000.

Pia inachimba visima 274 kwa ajili ya umwagiliaji wakulima wadogo 4,100 Geita, Kigoma, Tabora, Manyara, Dodoma, Mara, Pwani, Iringa, Singida, Mbeya, Morogoro, Njombe, Tanga, Mwanza na Arusha.

Inafungua viwanda vipya vya kuchakata chai Mlangali wilaya ya Njombe, Maruku Bukoba, Kibena Wanging'ombe, Ikanga Njombe, Luponde Ludewa na Itona Mufindi.

SEKTA ya mifugo na uvuvi imetoa chanjo kwa mifugo 2,239,755 kati ya Novemba, 2025 na Januari, 2026 ili kukinga mifugo dhidi ya magojwa.

Inajenga mabwawa 15 katika vituo vya kuendeleza ukuzaji viumbemaji vilivyopo Morogoro (Kingolwira10) na Igunga Tabora (Mwamapuli 5) ili kuongeza uzalishaji wa vifaranga na utoaji huduma za ugani.

Imeanza ujenzi wa soko la samaki Kipumbwi Tanga kwa Sh bilioni 1.3, ukikamilika utazalisha ajira 10,000.

Inaendelea na ujenzi wa bandari ya uvuvi Kilwa Masoko ambao hadi Januari 2026 umefikia asilimia 92 na unatakamilika Machi 2026 na kuzalisha ajira 30,000.

SEKTA ya viwanda na biashara, imefanikiwa kutoa mikopo 193 ya Sh milioni



1,085,900,000 kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi na Mfuko wa Kudhamini Mikopo kwa Wajasiriamali mikoa 19 ya Tanga, Tabora, Katavi, Pwani, Rukwa, Iringa, Morogoro, Ruvuma, Mwanza, Mbeya, Arusha, Kilimanjaro, Songwe, Shinyanga, Dodoma, Singida, Manyara, Kagera na Kigoma. Mikopo hiyo imezalisha ajira 265.

Aidha, mafunzo ya ujasiriamali yametolewa kwa vijana 1,200 na kusajili vijana 278 kwenye programu za uatamizi wa biashara.

Pia imerasimisha biashara kwa kusajili kampuni 4,233, majina ya biashara 7,498, kutoa leseni za viwanda 141 na kusajili alama za biashara na huduma 881 ili kuwalinda wabunifu.

Imetoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo 1,059 Dodoma, Iringa, Mwanza, Simiyu, Mara, Ruvuma, Arusha, Morogoro, Mwanza, Shinyanga, Geita, Pwani, Kagera, Kilimanjaro na Mtwara.

Inakamilisha tathmini ya awali ya kongani na mitaa ya viwanda katika mikoa ya Manyara, Singida, Mbeya, Iringa, Shinyanga, Ruvuma, Morogoro, Kilimanjaro, Dodoma, Tabora na Kigoma.

Imeanzisha programu maalum ya Ubora Kliniki. Kupitia programu hiyo, wajasiriamali wadogo na wa kati 1,059 katika mikoa 15 wamepata mafunzo SIDO bila malipo ya uzalishaji wa bidhaa bora na salama, uongezaji thamani, usimamizi wa biashara na masoko.

SEKTA ya Madini imepata mafanikio ya kukusanya Sh bilioni 311.80 ikiwa ni sawa na asilimia 111 ya lengo la kukusanya Sh bilioni 280.64 kati ya Novemba 2025 na Januari 25, 2026.

Imekamilisha Mkakati wa Uongezaji Thamani ya Madini wa miaka mitano 2026/2027 hadi 2030/2031. Pia imeongeza akiba ya dhahabu kwa kununua tani 17.03 za Sh Trilioni 4.97.

Imesimamia uuzwaji wa tani 14.66 za dhahabu za Sh trilioni 3.75 katika viwanda vya usafishaji dhahabu nchini.

Imechambua sampuli 19,705 za kijiolojia katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kufanya utafiti wa madini (QDS) 221 na 222 Kibiti na Rufiji na kuongeza eneo lililofanyiwa utafiti wa jiolojia kufikia asilimia 98.

Aidha, imesambaza makontena ya kuhifadhia na kuuzia mkaa safi Njombe, Mbeya, Songwe, Pwani, Dodoma, Iringa, Ruvuma, Geita na Shinyanga.

SEKTA ya Maliasili na Utalii imefanikiwa kuandaa mkakati mpya wa kitaifa wa kusimamia utatuzi wa migongano baina ya binadamu na wanyamapori wa miaka 10 (2025/26 – 2035/36) ili kulinda usalama wa wananchi na mali zao.

Imekamilisha taarifa ya matokeo ya sensa ya kitaifa ya wanyamapori nchi nzima ambayo imefanyika kwa mara ya kwanza baada ya miaka 10.

Pia imeandaa Mkakati wa Maendeleo Endelevu ya Utalii katika Ukanda wa Pwani na Baharini (2025 – 2035) unaolenga kukuza utalii wa fukwe na utamaduni kuanzia fukwe za Moa - Tanga hadi Msimbati – Mtwara.

SEKTA ya ardhi imefanikiwa kusajili hatimiliki 22,501, za kimila 31,459, za sehemu ya jengo 169 na nyaraka za kisheria 19,248.

Imetatua migogoro ya kiutawala 5,860 ambapo 2,116 imetatuliwa kupitia njia ya kawaida na 3,744 imetatuliwa kupitia kliniki za ardhi.

Imeidhinisha maombi 116 ya ardhi ya uwekezaji kwenye hekta 1,090.75. Maombi 32 ni ya raia na wanamiliki hekta 25.69 na 84 ni ya wawekezaji wanamiliki hekta 1,065.06. Uwekezaji wa nje mtaji una thamani ya dola za Marekani milioni 222.35.

Imejenga uwezo na kusajili wananchi 15,979 kwa ajili ya kutumia mfumo wa e-Ardhi kupata huduma za ardhi mahali popote.

Inaratibu uthamini wa mali za wananchi 1,800 kwa ajili ya malipo ya fidia katika mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) awamu ya Sita kipande cha kutoka Tabora hadi Kigoma kilomita 414.

Imeandaa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi na kufanya uhakiki na upimaji wa vijiji 40 katika halmashauri za Masasi (8), Kisarawe (8), Misungwi (8), Muheza (8), Mbeya (8) katika mikoa Mtwara, Pwani, Mbeya, Tanga na Mwanza.

Kuandaa na kutoa hati za Hakimiliki za Kimila 1,985 kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Taarifa za Matumizi Bora ya Ardhi (NLUIS) katika halmashauri za Sikonge (576), Ukerewe (773) na Nyanghwale (606).

SEKTA ya Nishati inaendelea na mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji 9,009 wa Sh trilioni 1.2 ambapo hadi Januari, 2026 vitongoji 39,888 kati ya 64,359 vimeunganishwa na umeme, sawa na asilimia 62.

Inakamilisha utekelezaji wa mradi wa kuzalishaji umeme wa megawati 50 kwa kutumia jua Kishapu, Shinyanga. Hatua inayofuata ni kufanya majaribio, ili uingizwe katika Gridi ya Taifa.

Pia inatekeleza miradi 235 ya kusambaza umeme kwa wateja kupitia Mpango Mahsusi wa Nishati na umeunganisha umeme wateja wapya 134,811.

Inatekeleza mkakati wa matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini ambao unalenga kuokoa mazingira, afya za watumiaji na muda.

Imewezesha taasisi 89 zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku kuanza kutumia nishati safi ya kupikia na kuachana na matumizi ya kuni na mkaa, hivyo kwa sasa taasisi 1,136 zinatumia nishati safi ya kupikia.

Imegawa kwa wananchi majiko banifu 13,575 yenye ruzuku ya asilimia 85 na mitungi ya LPG 28,653 ya kilo sita yenye ruzuku ya asilimia 50.

SEKTA ya ujenzi, imekamilisha ujenzi wa miradi 40 ya madaraja ya dharura kwa Sh bilioni 291.1.

Imekamilisha ujenzi wa barabara ya kilomita 1.5 ya kiwango cha Lami Mbeya.

Pia imesaini mkataba ujenzi barabara ya lami Makambako – Songea sehemu ya Rutukila– Songea kilomita 95.1 kwa Sh bilioni 158.67.

Imelipa Sh bilioni 105.876 kwa wakandarasi 133 waliojenga barabara na madaraja.

Inaendelea na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, miundombinu imekamilika na majengo yamefikia asilimia 67.94.

Inaendelea na miradi ya kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam, Mbeya na Dodoma.

SEKTA ya Uchukuzi, imekamilisha na kuzindua Meli ya New MV Mwanza Januari 23, 2026 ambayo inabeba abiria 1,200, tani 400 za mizigo, magari madogo 20 na magari makubwa matatu kwa wakati mmoja.

Pia inaendelea na maboresho ya Reli ya TAZARA mkataba wa ufufuaji na uboreshaji wa reli hiyo ulisainiwa Septemba 29, 2025 na kuzinduliwa Novemba 20, 2025 nchini Zambia.

Inaendelea na ujenzi wa matangi 15 ya mafuta katika bandari ya Dar es Salaam.

Inakamilisha ujenzi wa jengo la viongozi katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere – (Terminal I) litakalohudumia wakuu wa nchi watano kwa wakati mmoja.

Imekamilisha ujenzi wa bandari ya Kemondo na Bukoba katika ziwa Victoria ambayo ni kituo cha usafirishaji Bukoba, Mwanza na Bandari za Uganda.

SEKTA YA Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imekamilisha ujenzi wa minara 758 katika kata 713 kwa Sh bilioni 126 ambapo wananchi milioni 8.5 wamenufaika na mawasiliano ya simu na intaneti.

Vilevile, inajenga minara 636 vijijini (621 simu na 15 Redio), ujenzi wake umefikia asilimia 78 ikiwa ni ongezeko la asilimia 23 ikilinganishwa na asilimia 55 Oktoba, 2025.

Imesaini mkataba wa ujenzi wa minara ya simu 201 katika kata 201 zenye vijiji 263 Desemba 5, 2025 wa Sh bilioni 19.8. Mradi huo utanufaisha wananchi milioni 2.8.

Imeunganisha wilaya 10 katika Mkongo wa Mawasiliano ya Taifa za Kilwa, Maswa, Bariadi, Sikonge, Urambo, Ushirombo, Chunya, Karagwe, Nzega, na Butiama na kufanya wilaya 119 kati ya 139 ziwe

zimeunganishwa.

SEKTA YA Ulinzi na Usalama, mafanikio yaliyopatikana ni kuendelea kuimarisha hali ya ulinzi na usalama nchini pamoja na mipaka ya Tanzania.

Imeendelea kuimarisha ulinzi wa maeneo muhimu ya kimkakati kama mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere, Reli ya Kisasa (SGR), Mgodi wa Tanzanite Mirerani, Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanga, Mradi wa Kuchakata Gesi Asilia Likong'o Lindi, Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na viwanja vya ndege.

Kuendelea kushirikiana na Jumuiya za Kimataifa na Kikanda katika operesheni za ulinzi wa amani.

Imetambua na kusajili watu 117,002 hivyo kufanya watu waliosajiliwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kufikia 26,442,997. Aidha, vitambulisho vya NIDA 1,028 vimezalishwa na kufanya vitambulisho vilivyozalishwa kufikia 21,340,123.

Vilevile, Serikali imezalisha namba za utambulisho (NIN) 113,886 na hivyo kufikisha NIN 22,326,111 zilizozalishwa.

SEKTA ya Utumishi na Utawala Bora, imeajiri wahudumu wa afya 5,000 na walimu 7,000 ambao wamepangiwa vituo vya kazi na kuongeza utoaji huduma na kupunguza upungufu wa walimu wa sayansi.

Imeboresha mfumo wa e-Mrejesho utakaowezesha wananchi kutoa taarifa au malalamiko na kupata majibu.

SEKTA ya Utawala Bora imefanikiwa kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi 2,905 Morogoro na Singida ambapo migogoro 14 imetatuliwa kati ya 186 iliyopokelewa. Aidha, migogoro 172 imekabidhiwa kwa watendaji kwa ajili ya kutatuliwa.

SEKTA ya Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa imefanikisha mashauriano ya kimkakati na Jumuiya ya wanadiplomasia ndani na nje ya nchi kwa lengo la kulinda na kushamirisha taswira ya Taifa kikanda na kimataifa.

Imefikisha ujumbe maalum wa Rais Samia katika nchi za kimkakati zilizopo Amerika, Ulaya na Mashariki ya Kati unaofafanua mazingira chanya ya kisiasa, kiuchumi na kijamii nchini.

Imefanikisha mashauriano baina ya serikali na wabia wa maendeleo nchini kwa lengo la kushawishi nchi rafiki na mashirika ya kikanda na kimataifa kuendelea kushirikiana na Tanzania.

SEKTA ya Kazi, Ajira na Uhusiano imefanikiwa kuunganisha Watanzania 2,002 na fursa za ajira nje ya nchi na kuwezesha vijana 500 ambao ni madereva pikipiki kupata fursa za ajira Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Kuandaa mwongozo wa usimamizi wa mifuko ya hifadhi ya jamii kwa sekta isiyo rasmi ili kuongeza uwigo wa huduma za hifadhi ya jamii kwa wananchi waliojiajiri.

Imetangaza amri ya kima cha chini cha mshahara kwa sekta binafsi iliyoanza kutumika Januari, 2026, kwa lengo la kuboresha ustawi wa wafanyakazi.

Imezindua Kamati ya Majadiliano baina ya serikali, vyama vya wafanyakazi na waajiri kwa lengo la kuwa na uelewa na mtazamo wa pamoja, kupunguza migogoro na migongano baina ya wadau na kuongeza ufanisi na tija katika sekta ya kazi.

SEKTA ya Uratibu wa Mazingira imefanikisha kuhamisha taasisi 89 zinazolisha watu zaidi ya 100 kuanza kutumia nishati safi ya kupikia na kuachana na matumizi ya kuni na mkaa, hivyo kuwa na taasisi 1,136 zinazotumia nishati safi ya kupikia hadi sasa.

Pia imeshiriki mkutano wa 30 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC) uliowezesha nchi kupata ahadi ya dola za Marekani milioni 870 na Euro 500,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Imesajili miradi tisa ya biashara ya kaboni na hivyo kufikia miradi 82 iliyosajiliwa hadi Januari 2026.

SEKTA ya Maendeleo ya Jamii imetenga Sh bilioni 200 kwa ajili ya mitaji ya kuwezesha biashara ndogo, za kati na uendeshaji wa kampuni - changa ambazo zitanufaisha vijana katika sekta mbalimbali.

Mikopo mbalimbali imetolewa kwa wananchi kupitia vikundi mbalimbali kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu. Pia wafanyabiashara ndogo 1,054,149 wamesajiliwa na kupatiwa vitambulisho, nembo, vyeti na leseni za biashara. Vile vile wafanyabiashara ndogo 119,595 wamesajiliwa kupitia Mfumo wa WBN – MIS na kupewa vitambulisho.

Pia wajasiriamali wadogo na wadogo kabisa zaidi ya 3,900 wamepatiwa namba za mlipa kodi (TIN) na leseni za biashara.

Wachimbaji wadogo 2,239 wamerasimishwa kupitia wizara ya madini. Vikundi 1,216 vya makundi maalum vimesajiliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA). Kati ya hivyo, vikundi 1,123 vimepata zabuni za ununuzi za Sh 31,077,377,783.67 katika miradi ya umma kupitia sheria inayoelekeza asilimia 30 ya manunuzi ya umma kutengwa kwa makundi maalum.

Wafugaji 8,024 wamerasimishwa na kupewa mafunzo ya kilimo cha malisho, uboreshaji wa nyanda za malisho, afya ya mifugo na ya kilo 4,000 za vipando vya malisho kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI).

SEKTA ya Maendeleo ya Vijana inaimarisha ushiriki wa vijana katika utekelezaji wa Ajenda ya Maendeleo ya Taifa kwa kufanya majadiliano na vijana 8,120 katika maeneo ya uzalishaji mali Songwe, Mbeya, Ruvuma, Mtwara, Dar es Salaam na Dodoma ili kutatua baadhi ya changamoto zinazowakabili.

Pia imetenga Sh bilioni nane kwa ajili ya kutekeleza Programu za kipaumbele za Maendeleo ya vijana ambapo vijana 1,222 wanatarajiwa kunufaika.

KATIKA kudhibiti uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya, taasisi hiyo imekamata kilogramu 24,716.79 za dawa za kulevya na gramu 141.18 za dawa tiba zenye asili ya kulevya zikihusisha watuhumiwa 1,203.

Dawa za kulevya zilizokamatwa ni bangi kilogramu 18,616.065, Skanka 620.634, Mirungi 4,728.081, Heroin 574.029, Cocaine (5), Methamphetamine 172.8, MDMA 0.178, Flunitrazepam gramu 10.03, Pethidine 104.5, Morphine 4.65 na Fentanyl 22.

Pia ekari 112.8 za mashamba ya bangi 3,495 Tarime (Mara), Nzega (Tabora), Makete (Njombe) na Sengerema (Mwanza) zimeteketezwa. Pia zimeteketezwa kilogramu 1,030 za mbegu za bangi na kilogramu 812.46 za dawa za kulevya mirungi na bangi.

KATIKA Mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za udhibiti wa VVU na UKIMWI kwa kuongeza upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya kuimarisha udhibiti.

KATIKA kuratibu shughuli za maafa, zimenunuliwa boti mbili za kupambana na uharamia katika bahari na maziwa makuu. Boti hizo zitachangia kupunguza matukio ya uharamia na uhalifu, kuokoa maisha wakati wa dharura, kulinda mali za wananchi na kuchochea ukuaji wa kiuchumi katika maeneo ya bahari na maziwa makuu.

SEKTA ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya michezo kwa ajili ya mashindano ya AFCON 2027 ukiwemo uwanja wa mpira wa Arusha uliofikia asilimia 74 na ukarabati viwanja vya Benjamin Mkapa umefikia asilimia 95 na Uhuru asilimia 70.

## Hitimisho

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Samia imepata mafanikio makubwa kutokana na kutekeleza ahadi zilizotolewa wakati wa kampeni na ndani ya siku 100.






# DIRA 2050 Katika Kauli na Matendo

*Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kwenye hafla iliyofanyika ukumbi wa Jakaya Kikwete mkoani Dodoma. (Picha na Fadhili Akida)*

**Na Mwandishi Wetu**

TANGU kuapishwa kwake Novemba 2025 kuendelea kuliongoza Taifa katika awamu mpya, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameanza uongozi wake kwa kusisitiza kwa uthabiti ajenda ya maendeleo ya muda mrefu inayojengwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (DIRA 2050).

Katika kipindi cha siku 100 za mwanzo, mwelekeo wa Serikali umeonesha dhamira ya kuoanisha maamuzi ya sasa na mustakabali wa Taifa wa miongo ijayo.

Katika hotuba yake ya kulizindua Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mara baada ya kuapishwa, Mkuu wa Nchi alieleza kuwa muhula mpya unapaswa kuwa wa kasi, nidhamu na matokeo yanayopimika.

Alisisitiza kwamba Tanzania haiwezi kufikia hadhi ya uchumi wa kipato cha juu kwa kufanya maamuzi yasiyoangalia taswira ya muda mrefu. Alibainisha kuwa dira ya 2050 ni mwongozo wa kimkakati unaopaswa kuongoza upangaji wa bajeti, uundaji wa sera na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi zote za Serikali.

Mwelekeo wa Serikali katika kipindi hiki



*Mradi wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere umejengwa katika maporomoko ya mto Rufiji umekamilika na una uwezo wa kuzalisha umeme Megawati 2,115.*

unaonesha kuwa DIRA 2050 imechukuliwa kama nyenzo ya kuimarisha uchumi shindani na unaojitegemea. Msisitizo umewekwa katika kuongeza thamani ya rasilimali za Taifa, kuimarisha viwanda na kupanua wigo wa ajira.

Hoja ya kuondokana na utegemezi wa kuuza malighafi imeendelea kusisitizwa, kwa lengo la kuhakikisha kuwa rasilimali za nchi zinachangia kikamilifu katika mapato ya ndani na ustawi wa wananchi. Mwelekeo huu unalenga kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha uzalishaji na biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Katika siku 100 madarakani, Serikali imeendelea kuonesha kuwa miundombinu ni uti wa mgongo wa utekelezaji wa dira ya muda mrefu. Uwekezaji katika reli ya kisasa, uboreshaji wa bandari, upanuzi wa miundombinu ya barabara na kuimarisha upatikanaji wa nishati umeelezwa kuwa ni sehemu ya maandalizi ya uchumi wa viwanda na biashara ya kimataifa.

Kwa mtazamo wa kisera, uwekezaji huu si wa kizazi cha sasa pekee bali ni wa kuweka msingi wa ushindani wa Taifa katika miongo ijayo.

Aidha, rasilimali watu imeendelea kutajwa kama nguzo kuu ya mafanikio ya DIRA 2050. Rais Samia amesisitiza umuhimu wa kuimarisha elimu, hususan katika maeneo ya sayansi, teknolojia na mafunzo ya ufundi stadi.

Amebainisha kuwa uchumi wa kisasa unahitaji nguvu kazi yenye maarifa, ujuzi na ubunifu, na kwamba bila uwekezaji madhubuti katika sekta ya elimu, malengo ya muda mrefu hayawezi kufikiwa. Kwa mantiki hiyo, mageuzi ya elimu na uboreshaji wa mafunzo yanachukuliwa kama sehemu ya maandalizi ya uchumi wa maarifa unaotarajiwa kufikia mwaka 2050.

Sambamba na hilo, katika kipindi hiki siku 100, msisitizo umewekwa katika kuimarisha mazingira ya uwekezaji na ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Serikali ya Awamu ya Sita, imeelekeza nguvu katika kuboresha taratibu, kuongeza uwazi na kujenga imani kwa wawekezaji wa ndani na nje. Huu ni mkakati unaolenga kuifanya Tanzania kuwa kivutio cha mitaji, teknolojia na utaalamu unaohitajika katika safari ya kuelekea uchumi wa kipato cha juu.

Kwa upande wa utawala bora, kauli na mwelekeo wa Serikali umeunganisha kwa karibu DIRA 2050 na misingi ya uwajibikaji, nidhamu ya matumizi ya rasilimali za umma na uimarishaji wa taasisi za umma.

Ni dhahiri shahiri kuwa maendeleo ya muda mrefu hayawezi kupatikana bila utulivu wa kisiasa, mshikamano wa kitaifa na usimamizi thabiti wa sheria. Hivyo, ndani ya siku 100, Serikali imeendelea kusisitiza maadili ya uadilifu na uwazi kama sehemu ya kuimarisha imani ya wananchi na wadau wa maendeleo.

Vilevile, dhana ya maendeleo jumuishi imepewa uzito maalum. Mwelekeo wa sera umeonesha dhamira ya kuhakikisha kuwa wanawake, vijana na makundi maalum wanashiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi.

Uwezeshaji wa makundi haya unaonekana kama mkakati wa kupanua wigo wa uzalishaji, kuongeza ajira na kukuza kipato cha kaya. Hii inaendana na azma ya kujenga Taifa linalonufaisha wananchi wote bila kuacha mtu nyuma katika safari ya maendeleo.

Kwa ujumla, Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha pili, imeweka msingi wa kisera na kimkakati wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 unaolenga uthabiti wa sera, uwekezaji katika miundombinu na rasilimali watu, pamoja na kuimarisha utawala bora.

Kwa mtazamo wa uchambuzi wa maendeleo ya Taifa, hatua hizi za mwanzo zinadhihirisha dhamira ya kuifanya DIRA 2050 kuwa mwongozo hai wa ujenzi wa uchumi imara, unaojitegemea na unaowanufaisha wananchi wote.

Changamoto zilizopo zinahitaji ushirikiano mpana wa wadau wote wa maendeleo, lakini msingi uliowekwa katika siku 100 hizi unaashiria nia ya dhati ya kuijenga Tanzania yenye ushindani, ustawi na heshima katika jukwaa la kimataifa.




*Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akigawa kitabu kwa Rais Mstaafu wa awamu ya nne, Dkt. Jakaya Kikwete baada ya kuzindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kwenye hafla iliyofanyika ukumbi wa Jakaya Kikwete mkoani Dodoma. (Picha na Fadhili Akida)*

# Siku 100 za Rais Samia: Serikali yaonesha dhamira ya kuchochea mageuzi ya mashirika ya umma

Na Mwandishi wa OMH

DAR ES SALAAM. Tayari siku 100 zimepita tangu kuanza kwa awamu ya pili ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, huku Serikali ikiendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha ufanisi wa mashirika na taasisi za umma.

Katika kipindi hiki kifupi, jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita, muhula wa pili, zimeendelea kuimarika katika kuboresha utendaji wa mashirika ya umma kwa lengo la kuongeza tija, uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa uwekezaji wa Serikali.

Mwelekeo huu unaakisi maono ya Mhe. Rais Samia aliyoyatangaza bungeni wakati wa ufunguzi wa Bunge la 13, Novemba 14, 2025, ambapo alisisitiza dhamira ya Serikali kufanya mageuzi ya mashirika ya umma ili kuyawezesha kuwa na ufanisi zaidi na kuongeza mchango wake katika uchumi wa taifa.

Akihutubia Bunge hilo, Mhe. Rais alisema Serikali inalenga kuongeza si tu kiwango cha gawio kinachotolewa na mashirika ya umma, bali pia kuhakikisha taasisi na mashirika hayo yanachangia angalau asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Serikali ifikapo 2030.

"Nia yetu ni kuyajengea uwezo mashirika ya umma yaweze kushindana na kuwekeza nje ya Tanzania, kama mashirika mengine ya nje tunavyoyaona hapa nchini kwetu," alisisitiza Mhe. Rais.

Aliongeza kuwa mageuzi hayo ni sehemu ya jitihada pana za kuimarisha sekta ya umma na kuweka msingi madhubuti wa uchumi wa taifa, hatua itakayosaidia kufanikisha malengo ya maendeleo ya nchi katika miaka ijayo.

Katika utekelezaji wa maono haya, ndani ya siku 100 za mwanzo za awamu ya pili ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Samia, Ofisi ya Msajili wa Hazina (OMH) tayari imechukua hatua za kimkakati, ikiwemo kukamilisha Mpango Elekezi wa Muda Mrefu wa miaka 25 (2026–2050), unaolenga kuimarisha usimamizi wa uwekezaji wa Serikali katika mashirika ya umma.

Mpango huu wa OMH ni tafsiri ya moja kwa moja ya Dira 2050, ambayo inalenga kuifanya Tanzania kuwa na uchumi shindani na jumuishi unaochagiza ustawi wa wananchi, huku ikilenga pia kufikia thamani ya dola za Marekani trilioni 1 ifikapo mwaka 2050 kutoka takribani dola bilioni 85 za sasa.

Dira hii ndiyo mwongozo wa juu wa kimkakati unaoonesha njia ambayo Tanzania itafuata kufikia malengo haya katika kipindi cha muda mrefu.

Ili kutafsiri maono ya Dira 2050 kuwa hatua za utekelezaji, Serikali imetengeneza Mpango Elekezi wa Maendeleo ya Muda Mrefu (Long Term Perspective Plan – LTPP) kwa kipindi cha 2026/27 hadi 2050/51, ambao unaweka mikakati maalum ya sekta mbalimbali za uchumi itakayosaidia kufanikisha malengo hayo.

Mpango huo hutekelezwa kupitia Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27–2030/31, unaobainisha miradi, vipaumbele vya maendeleo na hatua za



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan*



*Msajili wa Hazina, Bw. Nehemiah Mchechu*

utekelezaji katika kipindi hicho.

Hatua hizi huungwa mkono na Bajeti za Serikali za kila mwaka, ambazo hutenga rasilimali fedha kulingana na vipaumbele vilivyowekwa katika mipango ya maendeleo ya Taifa, ikiwemo Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27.

Kupitia mfumo huu wa mipango, utekelezaji wa Dira 2050 unafanyika kwa hatua, kwa mpangilio na kwa ushiriki wa taasisi za umma, sekta binafsi na wadau wengine wa maendeleo.

Ni katika muktadha huo OMH, kama msimamizi wa uwekezaji wa Serikali katika mashirika ya umma, imeweka mkazo katika maeneo kadhaa ya kipaumbele ya kimkakati ndani ya Mpango wake Elekezi wa Muda Mrefu, yanayolenga kuongeza ufanisi, uwajibikaji na mchango wa mashirika ya umma katika uchumi wa taifa.

Taasisi inaendeleza jitihada za kuongeza mapato yasiyo ya kodi (NTR) ili kuongeza mchango wa mashirika ya umma katika bajeti ya Taifa na kufanikisha malengo ya maendeleo ya Taifa.

Aidha, OMH imedhamiria kuongeza ufanisi wa kiutendaji na utawala bora, ikirahisisha utendaji wa mashirika na kuimarisha uwajibikaji wa viongozi.

Taasisi pia inalenga kuwajengea uwezo viongozi, kwa kutoa mafunzo elekezi kwa wakuu wa taasisi, kuhakikisha viongozi wanatekeleza mageuzi kwa ufanisi na kuchochea tija katika mashirika yao.

Hali hiyo inaungwa mkono na jitihada za kuboresha matumizi ya mali za umma na faida itokanayo na uwekezaji 'return on investment', hatua ambazo tayari zimeanza kuzaa matunda.

Zaidi, OMH itaendelea kukumbatia ujumuishaji wa mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA)) ili kuboresha uratibu, mawasiliano na ufuatiliaji wa utendaji wa kifedha na kiutendaji wa mashirika ya umma.

Mageuzi yanayoendelea tayari yameanza kuonesha matokeo chanya ambapo baadhi ya mashirika ya umma yaliyokuwa na mitaji hasi au kupata hasara kwa muda mrefu sasa yameanza kujiendesha kwa ufanisi na kutoa gawio kwa Serikali.

Baadhi ya mashirika hayo ni pamoja na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

"Mashirika ya umma yanapaswa kujiendesha kwa misingi ya kibiashara na kutoa gawio kwa Serikali kwa kuwa Serikali imewekeza rasilimali nyingi ndani ya taasisi hizo," alisema hivi karibuni Mhe. Rais Samia.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais—Mipango na Uwekezaji, Mhe. Prof. Kitila Mkumbo, amekuwa akisisitiza umuhimu wa mashirika ya umma kuongeza ufanisi ili kuimarisha mchango wake katika




> **"Mashirika ya umma yanapaswa kujiendesha kwa misingi ya kibiashara na kutoa gawio kwa Serikali kwa kuwa Serikali imewekeza rasilimali nyingi ndani ya taasisi hizo," alisema hivi karibuni Mhe. Rais Samia.**

uchumi wa Taifa.

Mwezi Desemba mwaka jana alinukuliwa akizionya taasisi na mashirika ya umma yasiyoonesha ufanisi kuwa yapo hatarini kufutwa au kuunganishwa endapo hayataboresha utendaji wao.

"Ni afadhali kuwa na mashirika machache ya biashara, lakini yanayotoa gawio stahiki kwa Serikali," alisisitiza Prof. Mkumbo.

Akifafanua jinsi maono haya yanavyotekelezwa, Msajili wa Hazina, Bw. Nehemiah Mchechu, alisema Ofisi yake inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha usimamizi wa mashirika ya umma, kuhakikisha yanaongeza mchango wake katika mapato ya Serikali."

"Ofisi yangu inatambua kwamba pamoja na mafanikio yaliyooneshwa na taasisi za umma bado tuna kazi kubwa ya kuendelea kufanya maboresho ya kiutendaji na kiuendeshaji," alisema.

Aliongeza kuwa OMH itaendelea kuhakikisha idadi ya mashirika yanayochangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali inaongezeka, utegemezi wa ruzuku unapungua na mashirika yanayopata hasara yanaondoka katika kundi hilo.

"Tutaendelea kulinda uwekezaji wa umma kwa wivu mkubwa na kuhakikisha mashirika ya umma yanafanya kazi kwa ufanisi ili kuchangia kikamilifu katika uchumi wa taifa," alisisitiza.

Kupitia Mpango wake wa miaka 25, OMH imeweka malengo madhubuti ya kuongeza mchango wa mashirika ya umma katika Pato la Taifa kutoka asilimia 5 hadi asilimia 10 ndani ya kipindi cha miaka mitano.

Vilevile, Ofisi inalenga kuongeza mchango wa taasisi za umma kwenye mapato ya ndani ya Serikali kutoka asilimia 3.6 hadi asilimia 10 katika kipindi hicho.


OMH imejikita pia katika kukusanya Sh2 trilioni kama mapato yasiyo ya kodi kwa mwaka wa fedha 2025/26, ikizingatia mafanikio ya mwaka uliopita (2024/25) ambapo kiasi cha Sh1.028 trilioni kilikusanywa, hatua inayoonesha kuongezeka kwa mchango wa mashirika ya umma katika mapato ya taifa na kuthibitisha ufanisi wa sera na mipango ya uwekezaji wa Serikali.

Mbali na mafanikio ya siku 100, OMH inaendelea kuchukua hatua za muda mrefu ambazo zinasaidia utekelezaji wa maono ya Mhe. Rais na Dira 2050.

Hatua hizi ni pamoja na kutoa uhuru kwa mashirika 57 ya kibiashara na kimkakati kujiendesha ili kufikia ufanisi uliotarajiwa, kuunganisha na kufuta baadhi ya taasisi ili kuongeza tija, na kuboresha mizania ya taasisi kama ilivyofanyika kwa Benki ya Taifa ya Biashara (TCB) na TANESCO, hatua ambazo zilipelekea ongezeko la faida.

Aidha, kwa kushirikiana na Taasisi ya Uongozi, OMH imeendelea kutoa mafunzo elekezi kwa wakuu wa taasisi za umma, ambapo kati ya mwaka 2024 na 2025 mafunzo yalitolewa kwa wakuu wa taasisi 201, kuhakikisha viongozi wanatekeleza mageuzi kwa ufanisi na kuongeza mchango wa taasisi zao katika uchumi wa taifa.

Kwa ujumla, siku 100 za mwanzo za awamu ya pili ya uongozi wa Mhe. Rais Samia zimeonesha mwelekeo thabiti wa mageuzi katika usimamizi wa uwekezaji wa umma nchini.



# Siku 100 za uongozi wa Rais Samia zaifikisha Tanzania Hatua ya 16 Bora AFCON 2025

Na. WHUSM

Tangu kuingia madarakani kwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kumekuwepo na hatua kubwa za kuimarishwa kwa sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Sekta hizi zimeendelea kuwa chachu ya ajira, ukuaji wa uchumi, utalii, diplomasia na ustawi wa kijamii.

Kupitia dira na maamuzi ya kisera ya Rais Samia, sekta hizi zimepata uhalisia mpya unaojikita katika ubunifu, ushirikishwaji wa wananchi, weledi na maendeleo endelevu. Leo hii, sekta hizo ni mhimili wa furaha ya taifa, kiungo cha umoja wa kitaifa, na nyenzo muhimu ya kutangaza taswira chanya ya Tanzania kimataifa. Chini ya Awamu ya Sita, sekta hizi zimekuwa na msisimko mkubwa katika jamii kufuatia juhudi za Serikali kuimarisha mazingira rafiki ya kisera na kisheria. Hatua hizo zimeongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za kiuchumi, hususan vijana, ambao sasa wanaona fursa katika sekta hizi kama nyenzo ya kuinua uchumi binafsi na wa taifa kwa ujumla.

Uongozi wa Awamu ya Sita unafikisha siku 100 zikishuhudiwa mabadiliko makubwa katika sekta ya michezo. Sekta hii imeendelea kuliheshimisha taifa, ambapo Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanikisha mageuzi makubwa kuanzia miundombinu ya michezo, maandalizi ya timu, hadi ushiriki wa mashindano ya kimataifa.

Hivi karibuni, mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) 2025 yalifanyika nchini Morocco, ambapo Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi shiriki na kuonesha ushindani wa hali ya juu katika Kundi C lililojumuisha Nigeria, Uganda na Tunisia, na kufanikiwa kufuzu hadi hatua ya timu 16 bora.

Mafanikio hayo yametokana na juhudi kubwa za Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), ambazo zilihakikisha maandalizi bora ya timu kwa kuipeleka kambini nchini Misri pamoja na kupata mechi za kirafiki zilizosaidia kuimarisha uwezo wa timu. Ikumbukwe kuwa, Tanzania imeshiriki mashindano ya AFCON kwa mara ya nne tangu kuanzishwa kwake mwaka 1957, ikiwa ni baada ya kushiriki miaka ya 1980, 2019 na 2023.

Ushindi wa Taifa Stars katika mashindano hayo ulishuhudiwa na Watanzania wengi, ambapo kwa upande wa Wizara, Waziri Mheshimiwa Paul Makonda aliambatana na timu hiyo katika mashindano hayo. Akiwa katika kambi ya timu, alizungumza na wachezaji pamoja na benchi la ufundi na kuwasisitiza wachezaji kupambana kwa moyo wote, kuzingatia nidhamu na kuonesha uzalendo wanapovaa jezi ya Taifa. Alibainisha kuwa Watanzania wote wako nyuma yao, wakiendelea kuwaunga mkono, kuwashangilia na kuwaombea ili waliletee taifa heshima.

“Taifa zima lina imani kubwa nanyi. Chezeni kwa moyo, kwa umoja na kwa kujituma, mkijua mna mamilioni ya Watanzania wanaowaombea na kuwaunga mkono,” alisema Mheshimiwa Makonda.

Kauli hiyo iliitia hamasa kubwa kwa Taifa Stars ambao walipambana kwa hali ya juu na hatimaye kufuzu hadi hatua ya timu 16 bora. Mafanikio hayo yaliiongezea Tanzania heshima katika tasnia ya soka na kuiwezesha kupanda hadi nafasi ya 110 katika viwango vya ubora wa soka duniani.

Baada ya kufikia hatua hiyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliamua kuwapongeza vijana hao kwa kuwaandalia sherehe maalumu ya kuwapongeza iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam tarehe 10 Januari 2026. Katika hafla hiyo, Rais Samia alisema kuwa mafanikio ya Taifa Stars katika mashindano ya AFCON kwa mwaka huo yameiletea nchi heshima kubwa, na ni ushahidi tosha kwa dunia kuwa soka la Tanzania linaendelea kukua na kupanda viwango barani Afrika.

“Hongereni sana, mmefanya kazi nzuri sana. Tunajua kilichotokea na sababu zake, kwa kuwa walikuwa wenyeji, taifa lenye rasilimali na lenye ushawishi katika uandaaji. Hata hivyo, dunia imeona wazi kuwa Tanzania ina wapambanaji, na mmepambana kwa nguvu zenu zote. Nawapongeza sana,” alisema Rais Samia.

Ndani ya siku 100 za Dkt. Samia katika sekta ya michezo ulifanyika Mkutano wa Mwaka wa Shirikisho la Mpira wa Miguu barani Afrika uliofanyika Februari 13, 2026 ambao uliongozwa na Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), Dkt. Patrick Motsepe, na kukutanisha viongozi mbalimbali wa soka barani Afrika kujadili masuala muhimu ya maendeleo ya mpira wa miguu.

Uenyeji wa mkutano huo unaendelea kuonesha nafasi ya Tanzania katika ramani ya soka la Afrika, hususan katika kipindi hiki cha maandalizi ya mashindano ya AFCON 2027.





Chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia, dhana ya 'Goli la Mama' imekuwa chachu kubwa ya hamasa kwa wachezaji na klabu za mpira wa miguu nchini. Kupitia mpango huu, klabu zinapofanya vizuri katika mashindano ya kimataifa hupokea motisha ya kifedha moja kwa moja kutoka kwa Rais kama ishara ya kuthamini mafanikio yao. Ndani ya siku 100 za uongozi wa Awamu ya Sita, klabu za Young Africans (Yanga), Simba SC, Azam FC na Singida Black Stars zimekuwa miongoni mwa wanufaika wakubwa wa mpango huu.

Kazi kubwa ya ujenzi wa viwanja vipya vya michezo inaendelea kwa kasi katika mikoa ya Arusha na Dodoma. Uwanja wa Arusha umefikia zaidi ya asilimia 72 ya utekelezaji wa ujenzi na unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka huu, huku ujenzi wa Uwanja wa Dodoma ukiwa katika hatua za awali na ukitarajiwa kukamilika mwaka 2027.

Sambamba na hilo, Serikali imefanya maboresho makubwa katika Viwanja vya Leaders, Gymkhana II, FARASI, Jamhuri Morogoro na Mkwakwani Tanga, kwa lengo la kuvitumia kama viwanja vya mazoezi kwa timu za ndani na zile za wageni zitakazoshiriki mashindano ya kimataifa.

Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ambacho ni chuo pekee cha aina yake katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, hakikusahaulika katika mageuzi haya. Serikali inaendelea kukifanyia ukarabati mkubwa unaojumuisha uboreshaji wa hosteli za wanafunzi pamoja na ujenzi wa Akademia ya Michezo, inayolenga kutoa mafunzo ya kisasa na kuvutia vijana wengi zaidi kujiunga na chuo hicho. Aidha, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa vituo vya kupumzikia wananchi (recreation centres) katika Jiji la Dodoma na Dar es Salaam ili kuongeza maeneo ya burudani, mazoezi na kuimarisha ustawi wa jamii.

Mafanikio yaliyopatikana katika siku 100 za uongozi wa Awamu ya Sita yameonekana pia kupitia tuzo maalumu aliyopokea Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) ikiwa ni kutambua mchango wake mkubwa katika maendeleo ya soka nchini na barani Afrika kwa ujumla.

Kwa upande wa sekta ya habari, juhudi za Serikali kuhakikisha taaluma ya habari inasimamiwa kwa viwango vya juu zimeendelea kuonekana wazi baada ya kuundwa kwa Bodi ya Ithibati ya Wanahabari, chombo mahsusi chenye jukumu la kusimamia ubora, maadili na weledi wa wanahabari nchini. Bodi hiyo iliyozinduliwa rasmi mwaka 2025, imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa ithibati na vitambulisho kwa wanahabari waliokidhi vigezo vya kitaaluma, kusajili wanahabari, pamoja na kuhakikisha utekelezaji wa majukumu yao unazingatia kanuni, maadili na taratibu za taaluma ya habari.

Tangu kutangazwa rasmi kwa Siku ya Kiswahili Duniani, Tanzania imeendelea kuwa kinara katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Hivi karibuni, nyota ya Kiswahili imeendelea kuangaza kimataifa baada ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kuridhia lugha ya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha zitakazotumika rasmi katika Mikutano Mikuu ya shirika hilo.

Kauli hiyo ilitolewa katika Mkutano Mkuu wa 43 wa UNESCO uliofanyika jijini Samarkand, Uzbekistan, kuanzia tarehe 30 Oktoba na uliohitimishwa tarehe 13 Novemba 2025.

Tamko hilo rasmi la UNESCO lililotolewa tarehe 11 Novemba 2025, limetokana na maombi yaliyowasilishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA).

Kupitia Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara itaendelea kusimamia sera na mikakati ya sekta zake kwa lengo la kuhakikisha Watanzania wanaendelea kunufaika na fursa mbalimbali zinazotokana na wizara hiyo, ambayo ni miongoni mwa wizara zinazotoa mchango mkubwa katika uundaji wa ajira na maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini.





HONGERA KWA
UONGOZI
BORA
NSSF
Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye
Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
SIKU
100
www.nssf.go.tz
@NssfTanzania





# NSSF Yapata Mafanikio Ndani ya Siku 100 za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan

**Na Mwandishi Wetu**

Ndani ya siku 100 za Rais Dkt. Samia, NSSF imepiga hatua kubwa na ya kihistoria kwa kuzindua mpango maalum wa uchangiaji wa hiari kwa wananchi waliojiajiri uitwao Skimu ya Hifadhi (Hifadhi Scheme). Mpango huu unatarajiwa kufikia mamilioni ya Watanzania wanaoweza kuchangia lakini walikuwa nje ya mfumo wa Hifadhi ya Jamii.

Uzinduzi wa Mpango huo ulifanywa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi Ajira na Mahusiano), Mhe. Deus Sangu (Mb), tarehe 9 Februari 2026 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC). Mpango huu ni sehemu ya utekelezaji wa hatua muhimu katika maboresho ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii ndani ya siku 100 tangu kuapishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 3 Novemba 2025. Aidha, hatua hii ni sehemu ya mafanikio makubwa katika kutekeleza ahadi za Muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Sita kwa wananchi.

**Waliojiajiri Kujumuishwa katika Mfumo Rasmi**

Kwa miaka mingi, zaidi ya asilimia 80 ya nguvu kazi ya Taifa, hususan wananchi waliojiajiri, wamekuwa nje ya mfumo wa hifadhi ya jamii na hivyo kukosa kinga dhidi ya majanga kama uzee, ulemavu, kifo, upotevu wa kipato au magonjwa yanayoweza kupunguza uwezo wa kufanya kazi. Kuzinduliwa kwa mpango wa Skimu ya Hifadhi kwa wananchi waliojiajiri na wanaoweza kuchangia kunaziba pengo hilo la kihistoria.

Aidha, Mpango huo unatekeleza moja kwa moja Sera ya Taifa ya Kinga ya Jamii kwa kupanua ushiriki wa wananchi katika mifuko ya hifadhi ya jamii na kuhakikisha Watanzania wote waliopo katika sekta ya umma, sekta binafsi na waliojiajiri wanapata fursa sawa ya kujiunga, kuchangia na kunufaika na mafao ya hifadhi ya jamii.

**Skimu ya Hifadhi (Hifadhi Scheme) ni Nini**

Skimu ya Hifadhi ni Mpango wa Uchangiaji wa Hiari unaolenga wananchi waliojiajiri, wakiwemo wakulima, wafugaji, wavuvi, wachimbaji wadogo wa madini, wasanii, machinga, waendesha bodaboda, wajasiriamali wadogo na wa kati pamoja na makundi mengine.

Kupitia Mpango huu, wananchi wanaojiunga na kuchangia watanufaika na mafao ya pensheni ya uzee, pensheni ya ulemavu na pensheni ya warithi. Vilevile, watanufaika na mafao mengine ya muda mfupi yakiwemo mafao ya matibabu, mafao ya uzazi pamoja na huduma nyingine zinazotolewa na NSSF.

Mpango huu unamuwezesha mwananchi kujiandikisha bila gharama yoyote. Pia anatakiwa awe Mtanzania na mkazi wa Tanzania Bara, aliye na umri kati ya miaka 15 hadi 70 na asiwe mwanachama wa Mifuko mingine inayotoa mafao ya hifadhi ya jamii kwa sasa.

Kiwango cha chini cha uchangiaji ni Shilingi 30,000 kwa mwezi kwa mwanachama mmoja ambapo atapata mafao yote ya msingi ikiwa ni pamoja na huduma za matibabu. Aidha, kiwango cha chini cha uchangiaji kwa mwezi ni Shilingi 52,200 kwa mwanachama, mwenza wake na watoto wasiozidi wanne. Mwanachama anayeweza kuchangia kiwango cha juu anashauriwa afanye hivyo kwani mafao huongezeka kwa kadiri michango anayochangia mwanachama kwenye Mfuko inavyozidi kuongezeka.



*Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan*
*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano, Mhe. Deus Sangu (kulia) akimkabidhi Hati ya Usajili wa Hifadhi Scheme, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Bw. Masha Mshomba.*




*Uzinduzi wa Skimu ya Hifadhi AICC Arusha.*

"Kivutio kikubwa cha skimu hii ni namna inavyoweza kuwajumuisha wananchi mbalimbali kwenye uchangiaji kwa kuzingatia hali halisi ya vipato vyao, ambapo mwanachama anaweza kuchangia kwa siku, wiki, mwezi au msimu kulingana na uwezo wake. Mwananchi pia anaweza kuwasilisha michango kwa njia anayoipenda na rahisi kwake ikiwa ni pamoja na kupitia simu ya mkononi popote alipo," alisema Bw. Masha Mshomba, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF.

Pamoja na uzinduzi wa Skimu ya Hifadhi, Mfuko unaendelea kutoa elimu na hamasa kwa Watanzania waliojiajiri ili wajisajili na kuchangia kwenye Skimu hii muhimu. Wanachama wa Skimu ya Hifadhi walikuwa 509,839 hadi kufikia mwishoni mwa Februari 2026. Kama ilivyoelezwa awali, lengo la Mpango huu ni kuwafikia wananchi wote waliojiajiri na wanaoweza kuchangia.

**Serikali yaendelea Kufanya Maboresho katika Sekta ya Hifadhi ya Jamii**

Pamoja na uzinduzi wa mfumo wa Skimu ya Hifadhi kwa Wananchi waliojiajiri ndani ya Siku 100 tangu kuapishwa kwa Mheshimiwa Rais, kwa mujibu wa takwimu za Mfuko, hadi mwishoni mwa Desemba, 2025, thamani ya NSSF imeongezeka na kufika zaidi ya Shilingi trilioni 10.4, hatua inayoashiria ongezeko la uwezo wa kifedha na uendelevu wa Mfuko. Ukuaji huu wa Mfuko unaendelea kujenga imani ya wanachama kuhusu uimara wa Mfuko na uwezo wake wa kutekeleza majukumu ya msingi ikiwa ni pamoja na ulipaji wa mafao. Sababu kubwa iliyochangia ukuaji huo ni maboresho makubwa yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini. Maboresho haya yanachangia kwa kiasi kikubwa kwenye ongezeko la ajira, wanachama, michango, mapato ya uwekezaji na



*Waziri Deus Sangu OWM-KAM akishuhudia sukari ya viwandani inayozalishwa na kiwanda kipekee cha Mkulazi.*



*Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Bw. Masha Mshomba akitoa elimu ya hifadhi ya jamii kwa mwananchi aliyejiajiri katika soko la Tegeta Nyuki, Jijini Dar es Salaam.*



*Uwekezaji Kiwanda cha Mkulazi kinazalisha ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.*

hivyo ukuaji wa Mfuko.

Sambamba na mafanikio hayo, huduma za mafao zimeboreshwa ambapo kuanzia mwezi Februari 2026 wategemezi wa mwanachama walio na umri zaidi ya miaka 18 (au 21 kwa wanaosoma) sasa wananufaika na malipo ya mkupuo maalum pale mzazi mwanachama anapofariki, tofauti na awali ambapo hawakunufaika na mafao hayo.

Aidha, kuanzia Februari 2026 mwanachama aliyepoteza ajira na mwenye michango pungufu ya miezi 180 sasa anaweza kulipwa mafao yake yote kwa mkupuo (endapo ataridhia) baada ya miezi mitatu (siku 90) tangu kuachishwa kazi, tofauti na awali ambapo ilimlazimu kusubiri kwa kipindi kisichopungua miezi 24 (miaka miwili) kabla ya kulipwa mafao yake yote.

## Mafanikio ya Uwekezaji Mkulazi Yatajwa kuleta Tija

Mbali na mafanikio yaliyopatikana ndani ya siku 100 katika maboresho ya moja kwa moja ya sekta ya hifadhi ya jamii, Serikali kupitia NSSF na Jeshi la Magereza, imeendelea kuimarisha uwekezaji wa kimkakati katika kiwanda cha sukari cha Mkulazi. Tunafahamu kuwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alizindua rasmi kiwanda cha sukari cha Mkulazi tarehe 7 Agosti 2024 baada ya kuanza uzalishaji wa sukari ya majumbani Julai mwaka huo.

Ndani ya kipindi cha siku 100 cha Muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, tayari kiwanda kimeanza kuzalisha sukari kwa matumizi ya viwandani (white sugar). Hadi kufikia mwishoni mwa Februari 2026, kiwanda kimeweza kuzalisha ajira za moja kwa moja 2,172 na zisizo za moja kwa moja 8,000 na kufanya jumla ya ajira zilizozalishwa kufikia 10,172.

Mbali na kiwanda kuzalisha ajira, wakulima wa maeneo jirani wanapata nafasi ya kulima miwa na kuiuza kiwandani, jambo linalochangia kwa kiasi kikubwa kuwaongezea kipato, kuboresha maisha yao na kukuza uchumi wa maeneo jirani, mkoa pamoja Taifa kwa ujumla.

Hadi kufikia mwishoni mwa Februari 2026, kiwanda kimezalisha zaidi ya tani 45,594 za sukari ya majumbani na viwandani. Mbali na kiwanda kuzalisha sukari ya majumbani (brown sugar), kiwanda hiki ni cha kipekee na cha kwanza nchini kuzalisha sukari kwa matumizi ya viwandani (white sugar).

Kiwanda hiki pia kina uwezo wa kuzalisha megawati 15 za umeme, ambapo megawati saba (7) zitaingizwa kwenye gridi ya Taifa kupitia kituo cha Msamvu mkoani Morogoro. Megawati nane (8) zilizobaki ni kwa matumizi ya Kiwanda na shughuli nyingine kwenye mradi.

## Mtazamo wa Wananchi na Mweleko wa Siku 100

Baadhi ya wananchi waliojiajiri wameupokea Mpango wa Skimu ya Hifadhi kwa matumaini makubwa na wameelezea jinsi unavyotoa fursa ya kujiwekea akiba ya uzeeni pamoja na kuwa na uhakika wa maisha ya sasa na ya baadaye kutokana na uwepo wa kinga dhidi ya majanga mbalimbali yakiwemo ya upotevu wa kipato na gharama kubwa za huduma za afya.

Wananchi hao pia wameishukuru Serikali kwa kuendelea kuwekeza katika miradi inayogusa maisha yao moja kwa moja, ikiwemo mradi wa kiwanda cha sukari Mkulazi. Wamevutiwa mno na mchango wa kiwanda hiki katika kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja, jamii na Taifa kwa ujumla kupitia ongezeko la ajira, uzalishaji na fursa za biashara.

Aidha, wametoa shukrani kwa Serikali kwa maboresho ya kanuni za mafao, wakitaja kuwa ni hatua muhimu katika kuimarisha ustawi wa wanachama na wategemezi wao.


Wataalamu wa masuala ya kijamii wanaeleza kuwa ujumuishaji wa wananchi waliojiajiri katika mifumo ya hifadhi ya jamii ni mkakati muhimu unaowajengea wananchi utamaduni wa kujiwekea akiba, kuondoa umaskini, kuchangia katika ustawi wa uchumi na kuboresha maisha kwa ujumla.

## Hitimisho

Uzinduzi wa Skimu ya Hifadhi na Sera ya Taifa ya Kinga ya Jamii, maboresho mbalimbali yaliyofanyika pamoja na mafanikio yaliyopatikana ndani ya siku 100 za uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan yanaonesha dhamira ya Serikali katika kuimarisha ustawi wa wananchi kupitia mfumo jumuishi wa hifadhi ya jamii kwa wote. Hatua hizi zinaweka msingi wa kupanua wigo wa kinga ya jamii, kuondoa umaskini, kuimarisha ustawi wa wananchi na kuhakikisha hakuna Mtanzania anayeachwa nyuma tunapoendelea kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.



*Uwekezaji Kiwanda cha Mkulazi cha kuzalisha sukari ya viwandani na majumbani.*





*KUSHOTO: Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi (wa pili kushoto) akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Lazaro Twange (kushoto), akikagua Kituo cha Kupooza na Kusambaza Umeme cha Uhuru – Urambo chenye uwezo wa Megawati 24 pamoja na njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Urambo, kilichopo Mkoani Tabora. KULIA: Ujenzi wa matanki ya kuhifadhia mafuta katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki {EACOP} Chongoleani Tanga*

# Kutoka kwenye ahadi mpaka matokeo yanayowagusa wananchi kupitia sekta ya nishati

UONGOZI mahiri popote duniani hupimwa kwa uwezo wa kubadili ahadi kuwa vitendo vinavyogusa maisha ya wananchi kupitia utekelezaji wa miradi inayohakikisha upatikanaji wa huduma bora.

Ndani ya siku 100 za uongozi wa Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Watanzania wengi wameanza kuona ahadi zilizotekelezwa kwa vitendo katika Sekta ya Nishati.

Katika kipindi hiki kifupi, wananchi wanashuhudia majiko yasiyo na moshi yakiendelea kuongezeka, umeme ukiwaka hadi vitongojini, huduma bora za mafuta, huku gesi asilia nayo ikiendelea kuwa sehemu ya uzalishaji umeme, uendeshaji wa kuendesha viwanda na kutumiwa kwenye vyombo vya usafiri na majumbani.

Kwa upande wa Nishati Safi ya Kupikia, Rais Samia ameendelea kuwa kinara nchini na barani Afrika kwani ndani ya siku 100 kupitia Wizara ya Nishati amewezesha ugawaji wa majiko banifu 13,575 kwa ruzuku ya asilimia 85, majiko janja ya umeme (induction cookers) 7,292 pamoja na mitungi ya gesi ya LPG 27,153 ya kilo sita (6) kwa ruzuku ya asilimia 50 ambapo mitungi hiyo inapatikana kwa Mawakala wa Gesi katika Wilaya zote 139 nchini.

Juhudi hizi zimefanya idadi ya watumiaji wa Nishati Safi ya Kupikia kuongezeka hadi kufikia asilimia 23 ambapo matumizi ya nishati hii yanasaidia kulinda mazingira na afya za watumiaji.

Kwa upande wa taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 matumizi ya nishati safi ya kupikia yameongezeka na katika Siku 100 za Dkt. Samia Suluhu Hassan, taasisi 22 zimehamia kutumia nishati safi, hivyo kufikisha jumla ya taasisi 1,069 zinazotumia nishati safi ya kupikia.

Katika kuongeza wigo wa upatikanaji wa nishati safi ya kupikia, Serikali ya Awamu ya Sita imekamilisha ujenzi wa mitambo miwili ya kuzalisha mkaa mbadala katika Mikoa ya Dodoma na Tabora ambapo uzalishaji unatarajiwa kuanza mwezi Februari, 2026.

Aidha, baada ya kukamilisha upelekaji wa umeme katika vijiji vyote 12,318 nchini, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa kampeni za uchaguzi aliahidi kuwa ifikapo 2030 vitongoji vyote vitakuwa vimefikiwa na umeme.

Hili nalo halijabaki kwenye ahadi tu, kwani Serikali kupitia Wizara ya Nishati imeanza utekelezaji wa Mradi mkubwa wa Kupeleka Umeme katika vitongoji 9,009 wenye thamani ya shilingi trilioni 1.2. Tayari mikataba 30 imesainiwa kati ya Serikali na wakandarasi na kati ya hiyo mikataba 21 itatekelezwa na Kampuni za Wazawa.

Mradi huu ukikamilika utanufaisha wateja wa awali 290,300 katika mikoa 26 ya Tanzania bara. Mpaka sasa jumla ya vitongoji 39,888 kati ya 64,359 sawa na asilimia 62 tayari vimeunganishwa na umeme.

Katika kuimarisha uwezo wa ndani wa uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini, Serikali imekamilisha ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha nguzo za zege kinachomilikiwa na TANESCO mkoani Tabora. Kiwanda hiki kina uwezo wa kuzalisha nguzo 100 kwa siku na kinatarajiwa kuanza uzalishaji Februari, 2026. Hatua hii itaongeza kasi ya kuunganisha wateja wapya takribani milioni 1.7 kwa mwaka, sambamba na kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini.

Aidha, katika siku 100 za uongozi wa Rais Samia, Serikali pia imeendelea kuimarisha matumizi ya teknolojia kwa kuzindua matumizi ya Mita Janja za Umeme (Smart Meters). Hadi sasa, mita 47,341 zimefungwa kwa wateja mbalimbali nchini. Teknolojia hii inarahisisha ununuzi wa umeme, ambapo tokeni huingia moja kwa moja kwenye mita na kurejesha huduma mara moja pale umeme unapokatika.

Serikali pia imezindua mradi wa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Mtera kwa kufunga transfoma mbili zenye uwezo wa MVA 10 kila moja. Kukamilika kwa mradi huu kumetatua changamoto ya upotevu wa umeme na huduma isiyo ya uhakika katika Wilaya za Mpwapwa, Kongwa na Kilolo (Ismani), ambazo awali zilitegemea umeme kutoka umbali wa zaidi ya kilomita 155.

Kwenye sekta ya mafuta na gesi, Serikali imekamilisha maandalizi ya uchimbaji wa





*Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Salome Makamba (Katikati) akizindua awamu ya kwanza ya Mradi wa Kupeleka Nishati Safi ya Kupikia kwa Taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 katika shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kondoa mkoani Dodoma.*

visima vipya vinne vya gesi asilia, vitatu katika Kitalu cha Mnazi Bay mkoani Mtwara na kimoja katika Kitalu cha Ntorya mkoani Ruvuma ambapo uchimbaji unatarajiwa kuanza Februari, 2026.

Miradi hii inatarajiwa kuongeza uzalishaji wa gesi kwa kati ya futi za ujazo milioni 51 hadi 134 kwa siku katika kitalu cha Mnazi Bay, na futi za ujazo milioni 60 kwa siku kitalu cha Ntorya, hatua itakayochochea kukuza shughuli za kiuchumi na kijamii ambapo sasa, ajira 36 tayari zimetolewa katika hatua za maandalizi, huku zaidi ya ajira 400 zikitarajiwa kupatikana hadi kukamilika kwa miradi.

Serikali pia imeendelea kuimarisha usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini kwa kuongeza uwezo wa kuhifadhi mafuta katika Bandari ya Mtwara kutoka tani 29,280 hadi tani 110,221. Katika kipindi cha Novemba 2025 hadi Januari 2026, matumizi ya mafuta yalifikia lita 1,271,355,244 ikilinganishwa na lita 1,164,532,713 katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia, sawa na ongezeko la asilimia 9.2.

Sambamba na hilo, ujenzi wa ghala kubwa la kuhifadhi mafuta (Single Receiving Terminal) katika Bandari ya Dar es Salaam umefikia asilimia 30 na litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kuhifadhi tani 308,110.

Uendelezaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (EACOP) ni kielelezo kingine cha umahiri wa Serikali ya Awamu ya Sita kwani mradi huu unaendelea vizuri na umefikia asilimia 78.8, ambapo kilomita 521 kati ya 1,443 tayari zimeunganishwa na kufukiwa ardhini.

Mradi wa EACOP pia umeleta manufaa makubwa kwa Watanzania baada ya kutoa ajira 9,194 na kuwajengea uwezo wananchi 170 kupitia mafunzo ya viwango vya kimataifa. Aidha, zaidi ya kampuni 2,000 za Kitanzania zimenufaika kupitia ununuzi wa bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi trilioni 1.325, fedha ambazo zimechochea mzunguko wa uchumi wa Taifa.

Mwenye macho haambiwi tazama, hakika mafanikio ya siku 100 za uongozi wa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Sekta ya Nishati yanajionesha wazi huku yakiweka alama ya uongozi unaoweka maslahi ya wananchi mbele.



*Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius John Ndejembi, akibofya kitufe kuashiria uzinduzi wa mita janja za umeme kwa wateja . Kulia kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Salome Wycliffe Makamba, kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Jossen Mramba.*







*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akipata maelezo ya ufanisi wa majiko banifu pamoja na sufuria zake kutoka kwa Mkurugenzi wa Teknolojia Jadidifu na Nishati Mbadala, Mhandisi, Advera Mwijage kutoka REA; wilayani Muheza mkoani Tanga wakati wa Uzinduzi wa Usambazaji wa Nishati Safi ya Kupikia, Februari 27 mwaka 2025.*

# Mafanikio ya REA siku 100 za Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu**

NISHATI ni bidhaa na huduma muhimu katika maisha ya watu hasa katika kipindi hiki cha mapinduzi ya teknolojia na mabadiliko ya tabianchi.

Ni wakati huu dunia inahitaji nishati ya umeme na gesi asilia katika kudhibiti uharibifu wa mazingira na kupunguza ongezeko la joto ili kulinda tabaka la ozoni na kulinda dunia dhidi ya madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi yanayosababishwa na uharibifu wa mazingira.

Ni katika kulitekeleza hilo, Wakala ya Nishati Vijijini (REA) unafanya juhudi za kuhakikisha kila Mtanzania katika vitongoji na vijiji anapata umeme kama Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2025 – 2030 inavyoelekeza.

“Nawahakikishia kabla ya mwaka 2030 kwa kutekeleza ilani ya chama kilichoko madarakani, Chama Cha Mapinduzi kwamba ikifika mwaka 2030 vitongoji vyote viwe na umeme na mimi nakuhakikishia hilo litafanyika,” anasema Mkurugenzi Mkuu wa REA, Hassan Saidy.

Saidy ametoa ahadi hiyo alipozungumzia mafanikio ya siku 100 za uongozi za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi chake cha pili cha Serikali ya Awamu ya Sita.

Katika mahojiano maalumu hivi karibuni mkoani Dar es Salaam, Saidy alizungumzia ahadi ya kuwasha umeme katika vitongoji 9,000 vya mikoa 26 ya Tanzania Bara, na kwamba ahadi hiyo imeanza kutekelezwa kwa kusaini mikataba 30 ya miradi itakayotekelezwa na wakandarasi 17 wengi wao wakiwa ni wazawa.

Mikataba hiyo itatekelezwa kwa gharama ya Sh trilioni 1.2

Anasema kwa sasa tayari wakandarasi wamesharipoti katika mikoa husika kwa ajili ya kuanza kazi ya upimaji kabla ya kupeleka vifaa na kuanza utekelezaji.

“Ndani siku 100 za Mheshimiwa Rais tulisema tunaanza mradi mpya lakini tukizungumzia ndani ya kipindi chake cha miaka minne ile ya awali Wakala wa Nishati Vijijini tumetekeleza miradi minne ambapo tumefanikiwa kupeleka umeme vitongojini, karibu vitongoji 7,800 vilishaanza kufanyiwa kazi,” anasema Mkurugenzi Mkuu wa REA.

“Wakati anaingia madarakani vitongoji 36,000 vilikuwa havijafikishiwa huduma ya umeme, 28,000 ndiyo vilikuwa na umeme. Lakini ninavyozungumza hapa vitongoji takribani 41,000 vimefikishiwa umeme na tukipeleka hivi 9,000 itakuwa takribani vitongoji 50,000 kati ya 64,000 vitakuwa vimeshafikishiwa umeme,” anafafanua Saidy.

Anasema kwa kipindi cha miaka minne hali ya upatikanaji umeme vijijini imeimarika na hali ya kukatika imepungua kulinganisha na nyuma.

Anataja mafanikio mengine kuwa ni pamoja na kukamilika kwa Kituo cha Kupoza Umeme cha Mtera chenye uwezo wa kuzalisha zaidi ya megawati 20 pamoja kuanza kwa awamu ya kwanza ya mradi wa kuwezesha nishati safi kwa shule 53.

Anasema awamu ya pili mradi huo inatarajiwa kuanza hivi karibuni ikiwa na lengo la kufikisha mifumo bora ya nishati ya kupikia kwa taasisi 400.




Pia anasema REA imekamilisha mifumo ya kusambaza gesi asilia ya kupikia mkoani Lindi na Pwani, mradi utakaonufaisha wananchi 1,000 watakaounganishwa na huduma hiyo.

Anafafanua kuwa wakati mwingine umeme hukatika kutokana na hitilafu mbalimbali zinazojitokeza katika usafirishaji

Kuhusu baadhi ya vitongoji kurukwa na huduma ya umeme na kupelekwa maeneo ya mbele yake, Saidy anasema inatokana na vipaumbele vilivyowekwa na wakala.

“Wakati serikali inaanzisha REA tulikuwa tuna vipaumbele, lengo la msingi likiwa ni kila Mtanzania apate umeme lakini unaifikiaje hiyo azma kuna hatua za kuanza, wakati tunaanza ilikuwa dhamira ni kufikia mikoa, baadhi ya mkoa ambayo haijafikishiwa umeme inafikishiwa,” anabainisha.

Anasema baada ya kumaliza ngazi ya mkoa walifikia hatua ya kufikisha umeme katika makao makuu ya wilaya hali ambayo ilisababisha baadhi ya vijiji kupitiwa na umeme kuelekea wilayani lakini vyenyewe vikakosa umeme kwa kuwa mradi ulizingatia azma ya kufikisha kwenye makao makuu ya wilaya.

Anafafanua kuwa baada ya hatua hiyo walienda ngazi ya vijiji na hatimaye sasa wanatekeleza miradi ya vitongoji huku akieleza kuwa watafika mpaka ngazi ya chini ya kaya kwa kaya.

"Tulivyomaliza tukaenda vijijini lengo ni ndani ya makao makuu ya vijiji kuwe na umeme tunapotoa umeme kwenda kwenye tarafa bila shaka hapo katikati kuna kitongoji tutakuwa tumekipita, dhamira ni kuhakikisha kwanza ufike kijijini ili kazi ya kupeleka kwenye vitongoji ifate," anasema Saidy.

Anasema kwa hatua ya sasa ya vitongoji hakuna atakayerukwa.

Anasema mbali na kusaidia kufikisha umeme vijijini, miradi ya REA inanufaisha jamii za vijiji husika kwa kuwapatia ajira wakati wa utekelezaji wake.

Anasema kwa mradi wa vitongoji uliosainiwa hivi karibuni takribani vijana 4,600 watapata nafasi ya kufanya kazi katika maeneo ya miradi.

"Hizo ni kazi za kwenye maeneo ya miradi bado wale wa ofisini wa kufanya mahesabu, kuchora, hiyo ni ya kwanza. Lakini ya pili ndani ya vijiji tumetoa maagizo kwa wakandarasi wanapokwenda kufanya kazi kwenye vijiji zile kazi ambazo hazihitaji utaalamu zote zifanywe na wananchi wa maeneo ambayo mradi unatekelezwa," anaeleza Mkurugenzi Mkuu wa REA.

Anataja fursa nyingine zinazoweza kujitokeza ni pamoja na biashara ya chakula (wapishi), nyumba za kulala na maeneo ya kutunzia vifaa.

Aidha, anasema kitendo cha serikali kuwasogezea wananchi huduma za umeme karibu ni kuwafungulia fursa mpya za uchumi katika vijiji vyao na hivyo kupunguza changamoto ya uhaba wa ajira vijijini.

Akizungumzia usambazaji wa umeme katika visiwa, Saidy anaeleza: "Kwa wananchi walioko kwenye visiwa vidogovidogo wote watapatiwa umeme. Mpaka sasa visiwa 72 vimepatiwa umeme na visiwa 71 serikali inavifanyia kazi".

"Mradi ambao tumeuzindua ndani ya siku mia za Mheshimiwa Rais ni kupeleka umeme kwa kaya 20,000 katika visiwa 71," anaongeza.

Kuhusu nishati mbadala, anasema serikali kupitia REA inatoa ruzuku kwenye miradi ya gridi na ya nishati jadidifu ikiwamo umeme wa jua, wa upepo, wa tungamo taka na ule wa joto ardhi, miradi inayotekelezwa kwa kushirikiana na sekta binafsi.

"Huwa tunawezesha kwa namba tatu; ya kwanza tunatoa ruzuku katika hatua za awali, ya pili ruzuku ya matokeo na tatu ni mikopo ya masharti nafuu," anasema.

Mkurugenzi Mkuu wa REA anasema kuwa uko Mfuko wa Nishati Vijijini ambao unasaidia wazalishaji wadogo ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kupata mkopo wa riba nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

"Tuna gridi ndogo takribani 70 ambazo zinapata ufadhili kutoka Mfuko wa Nishati Vijijini watu wanazalisha umeme na wanatoa huduma, tunapozungumza hapa tumemaliza umeme kwenye vijiji na vitongoji, lakini kuna vijiji karibu 100 vinapata umeme kutoka kwa wazalishaji wadogo wanazalisha wenyewe na wanasambaza na hivyo vyote vimepata ufadhili wa serikali kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini," anabainisha maendeleo hayo ya sekta ya nishati.

Akizungumzia kasi ya kuhakikisha wanawafikia Watanzania kwa huduma za umeme, Saidy anasema katika kipindi cha miaka minne kasi ya kupeleka umeme vijijini imeongezeka kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na awali ambapo jumla ya 23,000 vimefikiwa na huduma ndani ya kipindi hicho.

"Nawahakikishia kabla ya 2030 kwa kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwamba ikifika 2030 vitongoji vyote viwe na umeme na mimi nawahakikishia hilo litafanyika," anasema Saidy, akisisitiza ahadi yake kwa wananchi ambao vitongoji vyao havijafikiwa na huduma za umeme mpaka sasa.

Kuhusu gharama za kunganishiwa umeme kupitia miradi ya REA, Saidy anaweka wazi kuwa ni Sh 27,000 kwa kila mtu kwa maeneo yote yenye miradi ya REA.

Hata hivyo, anasema pamoja na mafanikio hayo bado ziko changamoto zinajitokeza katika kutekeleza miradi ya REA ambazo ni pamoja na wananchi kukosa mwamko wa kuomba huduma za umeme zinapowafikia kwa kile anachosema wananchi wamekuwa hawaoni umuhimu wa kuomba.

Anataja changamoto nyingine kuwa ni za kimazingira hasa kwa kuwa nchi yetu ni kubwa na maeneo yote yanaishika hali inayofanya watu kusambaa katika maeneo mbalimbali na kufanya hali ya usambazaji kuwa kubwa zaidi.

Aidha, anasema iko changamto ya uharibifu wa miundombinu ambayo inasababisha hitilafu katika maeneo ya vijiji vinavyohudumiwa.

"Napenda kuwaambia Watanzania wote kwamba hii miundombinu ni yetu sote, imejengwa na serikali, lakini mwenye miundombinu ni mwananchi wa eneo husika," anasema Saidy.

Anaongeza: "Ukiona serikali imeweka transfoma ujue ni sawa na kuweka jenereta nyumbani kwako, mwisho wa siku huweki jenereta kuonekana una jenereta ila uweze kupata umeme, uweze kufanya shughuli zako zinazohitaji umeme".



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akiangalia teknolojia mbalimbali za nishati safi yakiwemo majiko banifu wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Usambazaji wa Nishati Safi ya Kupikia wilayani Muheza mkoani Tanga, tarehe 27 Februari, 2025.*



# TANESCO yaanika mafanikio lukuki uongozi wa Rais Samia

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) ni kampuni ya umma inayomilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo majukumu yake ya msingi ni uzalishaji wa umeme, usafirishaji wa umeme, na usambazaji wa umeme Tanzania Bara pamoja na Tanzania Zanzibar.

Wizara ya Nishati kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) imepitia mapinduzi makubwa chini ya uongozi wa Awamu ya Sita wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu alipoingia madarakani mwaka 2021.

Yapo mengi yanayoweza kuonesha hali ya umeme nchini kuanzia kwenye mafanikio yaliyopatikana kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme pamoja na mapato na maboresho ya huduma kwa wateja.

Mafanikio katika uzalishaji umeme

Hali ya uzalishaji umeme nchini imeimarika kwa kiwango kikubwa na hii ni baada ya kukamilika kwa miradi mbalimbali ya vyanzo vya uzalishaji umeme ambapo hadi kufikia mwezi Februari 2026 uwezo wa mitambo ya kufua umeme kwenye Gridi ya Taifa ulifikia jumla ya megawati 3,975.5 wakati mahitaji ya juu kabisa ya umeme kwenye Gridi ya Umeme ya Taifa yakiwa ni megawati 2071.3.

Katika kutambua mafanikio katika eneo la uzalishaji umeme, Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ni miongoni mwa mafanikio hayo makubwa.

Huu ni moja ya miradi kielelezo ya kufua umeme kwa njia ya maji kuwahi kutekelezwa hapa nchini ukiigharimu serikali jumla ya Shilingi trilioni 6.5. Kupitia mradi huu ndipo kulikozaliwa Kituo cha Kufua Umeme cha Julius Nyerere chenye uwezo wa kuzalisha jumla ya megawati 2,115 kilichokuja kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme nchini na kuifanya Tanzania kuwa na umeme wa uhakika.

Chakufahamu hapa ni kwamba wakati Mheshimiwa Rais Dkt. SamiaSuluhu Hassan akiingia madarakani Machi 2021, aliukuta mradi huu ukiwa asilimia 33 tu, lakini mpaka kufikia Februari 2026 mradi mpaka sasa umekamilika, jumla ya mitambo tisa (9) tayari inazalisha umeme.

Aidha, ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Chalinze ambacho ni sehemu ya mradi huo umekamilika kwa asilimia 100 ambapo ukamilishwaji wa miundombinu hii umewezesha umeme kusafirishwa kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha JNHPP hadi Chalinze na kuingizwa kwenye Gridi ya Umeme ya Taifa.

Sehemu nyingine muhimu katika Mradi wa JNHPP ni utekelezaji wa Mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka JNHPP hadi Chalinze kwa msongo wa kilovoti 400, yenye urefu wa kilometa 160 ambao umekamilika kwa asilimia 100.

Mradi mwingine ni Mradi wa Kufua Umeme kwa Maji wa Rusumo. Mradi huu ulitekelezwa kwa ushirikiano wa mataifa matatu ya Tanzania, Burundi na Rwanda ambapo umekamilika kwa asilimia 100 huku Tanzania ikipata wastani wa megawati 26.7 kati ya 80 zinazozalishwa ikiwa ni mgawanyo sawa kwa mataifa yote matatu.

Mbali na hayo, mradi huu umetoa fursa ya mtandao wa Gridi ya Taifa ya Tanzania kuungana na mitandao ya gridi za umeme za nchi za Burundi na Rwanda.

Mradi wa Malagarasi ni miongoni mwa miradi inayotekelezwa na TANESCO ya kuzalisha umeme. Mradi huu unatarajiwa kuzalisha jumla ya megawati 49 ambapo utaimarisha hali ya upatikanaji wa umeme hasa katika Mkoa wa Kigoma, lakini pia kwenye mikoa ya Magharibi mwa Tanzania. Kazi inaendelea katika mradi huu na hadi sasa umefikia asilimia za utekelezaji 22.72.

Mradi mwingine ni ule wa kuzalisha umeme kwa njia ya Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension. Mradi huu wenye uwezo wa kuzalisha megawati 185 umekamilika kwa asilimia 100 na tayari unachangia megawati 185 katika Gridi ya Taifa.


Katika kuongeza vyanzo vya uzalishaji umeme na kuondoa utegemezi wa maji na gesi, TANESCO imeendelea na ajenda ya kuzalisha umeme kupitia vyanzo mseto.

Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni pamoja na mradi wa kuzalisha umeme wa jua wa Kishapu. Mradi huu uko katika hatua za mwisho kwa awamu ya kwanza ambapo jumla ya megawati 50 zitazalishwa ambapo awamu ya pili ya utekelezaji wake jumla ya megawati 100 zitaongezeka na hivyo kufanya mradi huu kuzalisha megawati 150.

## Mafanikio usafirishaji umeme

Yapo mengi ya kujivunia. Katika upande wa usafirishaji umeme, TANESCO imefanikiwa katika usafirishaji umeme ikiwamo kuunganika kwa Gridi za Taifa katika Ukanda wa Afrika Mashariki ambapo imefanikiwa kuunganisha Gridi za umeme za Taifa kati ya Kenya na Tanzania kufuatia kukamilika kwa







*Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius John Ndejembi, akibofya kitufe kuashiria uzinduzi wa mita janja za umeme kwa wateja. Kulia kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Salome Wycliffe Makamba, kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Jossen Mramba.*

Mradi wa Kituo cha Kupoza na Kusafirisha Umeme cha Lemuguru kilichopo Arusha.

Muunganiko huu umekamilika na gridi kuunganika kwa kupitia laini ya usafirishaji umeme kutoka Arusha, Tanzania kwenda Kenya. Hatua hii inaifanya Tanzania kuwa katika Muunganiko wa Kikanda wa Nchi za Afrika Mashariki katika Umeme (Eastern Africa Power Pool).

Eneo jingine ni pamoja na utekelezaji wa Mradi wa Usafirishaji wa Umeme kutoka Tanzania hadi Zambia (TAZA) ambapo Tanzania itaungana na mtandao wa Gridi wa Jumuiya ya Nishati katika Ukanda wa Kusini mwa Afrika (Southern Africa Power Pool - SAPP).

Mradi huu unahusisha njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga (TAZA) yenye urefu wa kilometa 624 pamoja na vituo vyake vya kupoza umeme katika maeneo hayo. Utekelezaji wa mradi huu unaendelea na hadi sasa umefikia asilimia 74.

Mradi mwingine wa kusafirisha umeme ni ule wa njia ya kusafirisha umeme wa Chalinze hadi Dodoma. Mradi huu wa njia ya msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilometa 345, pamoja na upanuzi wa vituo vya kupokea, kupoza na kusafirisha umeme vya Zuzu Dodoma na Chalinze Pwani, unatarajiwa kukamilika Septemba mwaka huu 2026 ambapo kwa sasa ujenzi wake umefikia asilimia 50.

## Mafanikio huduma kwa wateja

Eneo la huduma kwa wateja ni moja ya eneo muhimu tunapoangazia mafanikio ya shirika. TANESCO imeendelea kuimarisha eneo hili katika kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na huduma ya umeme wa uhakika na kutatuliwa changamoto zozote zinazohusu huduma hiyo kwa urahisi na unafuu.

Katika eneo hili, TANESCO ilianzisha mita janja (smart meter) ambazo zinamfanya mteja kununua umeme na kuingia moja kwa moja pasipo kuingiza namba za tokeni katika rimoti. Mfumo huu ambao bado unaendelea kusambazwa kwa wateja nchini unazidi kuondoa kero na usumbufu wakati wa ununuzi wa umeme ambapo mteja anaweza kununua umeme popote pale alipo.

Ili kumfikia mteja kwa urahisi na kumhudumia shirika liliongeza vyombo vipya vya usafiri yakiwemo magari, pikipiki pamoja na bajaji zinazotumika kwa ajili ya kumfikia mteja popote pale alipo. Magari 240, pikipiki 320 na bajaji 219 vimenunuliwa ambapo sasa wateja wanaunganishiwa huduma ya umeme na kutatuliwa changamoto zao kwa wakati kila kona ya nchi bila ya uwepo wa kikwazo cha usafiri.

## Nishati safi ya kupikia

Kama mzajilishaji wa nishati ya umeme, TANESCO imeendelea kuhamasisha wananchi juu ya faida mbalimbali za kutumia nishati safi ya kupikia ya umeme ambapo shirika licha ya kutoa elimu kwa wananchi, lakini pia limeanzisha programu ambapo wafanyakazi wa shirika wanaweza kukopeshwa majiko sanifu ya umeme. Hii inaakisi msemo wa Kiswahili usemao 'Kizuri kinaanzia kwako" ambapo TANESCO imeonesha kwa vitendo dhamira yake ya wazi ya kuhakikisha Watanzania wanaitumia na kuiamini nishati ya umeme kupikia.

Lakini pia wateja na wananchi hawakuachwa kwani kuna programu ya kuwaunganishia umeme na kuwapatia majiko ya umeme ambapo wanapata fursa ya kulipia gharama za jiko kadri wanavyonunua umeme.

Yapo mengi ambayo Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linayahesabu kama mafanikio chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.








# Taarifa Fupi ya TPDC kwa Siku 100 za Rais Dkt. Samia





SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ni kampuni ya umma inayomilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Shirika hili lilianzishwa mwaka 1969 kwa Sheria ya Bunge kwa lengo la kusimamia, kuendeleza na kushiriki kwa niaba ya Serikali katika shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini.

Majukumu yake makuu ni pamoja na kusimamia mikataba ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi (Production Sharing Agreements – PSAs), kuendeleza miundombinu ya gesi asilia, kuhakikisha ushiriki wa wazawa (local content), pamoja na kulinda maslahi ya taifa katika rasilimali za petroli.

Chini ya uongozi wa Awamu ya Sita wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, sekta ya mafuta na gesi kupitia TPDC imeendelea kupata msukumo mpya wa kimkakati, ikilenga kuifanya rasilimali ya gesi asilia kuwa mhimili wa maendeleo ya uchumi wa viwanda, ajira na ustawi wa wananchi.

## Mafanikio katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za gesi

Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye akiba kubwa ya gesi asilia katika ukanda wa Afrika Mashariki. Ndani ya kipindi cha siku 100 za mwanzo wa muhula mpya wa Rais Samia, TPDC imeendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali hii kwa kuhakikisha mikataba ya utafutaji na uzalishaji inasimamiwa kwa uwazi, weledi na kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa.

Serikali imeendelea kusisitiza matumizi ya gesi asilia kama nishati safi na nafuu kwa uzalishaji wa umeme, matumizi ya viwandani na majumbani. Hatua hii imechangia kupunguza gharama za uzalishaji, kuongeza ushindani wa bidhaa za ndani na kukuza Pato la Taifa.

Aidha, TPDC imeendelea kuratibu na kusimamia miundombinu ya usafirishaji wa gesi ikiwemo mabomba ya gesi kutoka maeneo ya uzalishaji hadi vituo vya kuchakata na kusambaza gesi kwa matumizi mbalimbali nchini.

## Mafanikio katika miundombinu ya gesi asilia

Katika kuimarisha sekta hii, TPDC imeendelea kusimamia na kuboresha miundombinu ya gesi asilia ikiwemo bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam, ambalo limekuwa uti wa mgongo wa upatikanaji wa gesi kwa ajili ya kuzalisha umeme na kuendesha viwanda.

Miundombinu hii imewezesha upatikanaji wa gesi kwa uhakika katika maeneo ya viwanda, hususan jijini Dar es Salaam na mikoa jirani, na hivyo kuchochea ukuaji wa sekta binafsi na uwekezaji wa viwanda vipya.

Sambamba na hilo, Serikali kupitia TPDC imeendelea na majadiliano na maandalizi ya









*PICHA ZA JUU: Mitambo ya kuchakata gesi asilia iliyopo Madimba mkoani Mtwara na Songosongo mkoani Lindi. PICHA ZA CHINI: Mitambo ya kusafirisha gesi asilia iliyopo Somangafungu wilayani Kilwa mkoa wa Lindi.*

miradi mikubwa ya kimkakati ya gesi asilia iliyolenga kuongeza thamani ya rasilimali hii kwa manufaa ya muda mrefu ya Taifa.

## Mchango wa sekta ya mafuta na gesi katika uchumi

Ndani ya siku 100 za mwanzo wa muhula mpya, sekta ya mafuta na gesi imeendelea kuchangia mapato ya Serikali kupitia tozo, gawio na kodi mbalimbali zitokanazo na shughuli za uzalishaji na usambazaji wa gesi.

Gesi asilia imeendelea kuwa chanzo kikuu cha uzalishaji wa umeme nchini, hatua iliyosaidia kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa viwanda, taasisi na wananchi kwa ujumla. Hii imeleta athari chanya katika sekta za viwanda, biashara, huduma na ajira.

## Uwazi, uwajibikaji na ushirikishwaji wa wazawa

Katika hotuba yake ya tarehe 14 Novemba 2025 bungeni jijini Dodoma, Rais Samia alisisitiza kuwa rasilimali za mafuta na gesi ni mali ya Watanzania wote na zinapaswa kusimamiwa kwa uwazi na uwajibikaji.

Ndani ya siku 100 hizi, TPDC imeendelea kuimarisha ushiriki wa Watanzania katika sekta hii kupitia sera ya ushirikishwaji wa wazawa (local content), kwa kutoa fursa kwa wataalamu wa ndani, wakandarasi wazawa na kampuni za Kitanzania kushiriki katika miradi ya mafuta na gesi.

Hatua hii inalenga kujenga uwezo wa kitaifa, kuongeza ajira kwa vijana na kuhakikisha kuwa utaalamu na teknolojia vinabaki nchini kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

## Uwajibikaji kwa jamii (CSR)

TPDC imeendelea kutekeleza miradi ya kijamii katika maeneo yanayozunguka shughuli za uzalishaji wa gesi asilia. Kupitia sekta za elimu, afya, maji na miundombinu, wananchi wameendelea kunufaika moja kwa moja na uwepo wa rasilimali hizi.

Hii inaendana na maelekezo ya Serikali ya Awamu ya Sita kwamba maendeleo ya rasilimali lazima yaonekane katika maisha ya wananchi wa kawaida.

## Ulinzi wa mazingira na usalama

Serikali chini ya Rais Samia imeendelea kusisitiza kuwa maendeleo ya kiuchumi hayawezi kupatikana kwa gharama ya mazingira. Kwa hiyo TPDC imeendelea kusimamia shughuli zote za utafutaji, uzalishaji na usafirishaji wa gesi kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa vya uhifadhi wa mazingira, afya na usalama kazini.

Yapo mengi ambayo TPDC inayahesabu kama mafanikio ndani ya siku 100 za mwanzo wa muhula mpya wa Rais Samia Suluhu Hassan. Kupitia usimamizi madhubuti wa rasilimali za gesi asilia, uimarishaji wa miundombinu, kuongezeka kwa ushiriki wa wazawa na uwajibikaji kwa jamii, sekta ya mafuta na gesi imeendelea kuwa nguzo muhimu ya maendeleo ya Taifa.

Ki ukweli sekta hii imechangia pakubwa katika kuimarika kwa uzalishaji wa umeme, kukuza viwanda, kuongeza ajira na kuimarisha mapato ya Serikali.

TPDC bado ipo kazini! Inaendelea kuhakikisha kuwa rasilimali za mafuta na gesi zinakuwa baraka kwa Watanzania wote, leo na kwa vizazi vijavyo.








*Mtambo unaotumika kuchimba visima vya gesi asilia katika Kitalu cha Mnazi Bay Mkoani Mtwara.*

# Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha siku 100 cha uongozi wa Rais Samia



*Mhandisi Yoctan Magazi kutoka PURA katika zoezi la ukaguzi na majaribio ya mtambo wa uchimbaji wa visima vya gesi asilia.*

**UTANGULIZI**

Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 ikiwa na jukumu la kusimamia na kudhibiti shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini.

Aidha, PURA ina jukumu la kuishauri Serikali kuhusu sera na mikakati ya maendeleo ya rasilimali za mafuta na gesi, pamoja na kusimamia maendeleo ya Mradi wa Kuchakata Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG Project) kwa ajili ya mauzo ya nje.

Katika kipindi cha siku mia moja (100) za uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, PURA imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio makubwa katika kuimarisha maendeleo ya sekta ya mafuta na gesi nchini.

**MAFANIKIO MAKUU YALIYOPATIKANA**

Maandalizi ya Uchorongaji wa Visima Vipya vya Gesi Asilia

PURA imesimamia maandalizi ya uchorongaji wa visima vinne (4) vya gesi asilia, ambapo visima vitatu (3) vitachorongwa katika Kitalu cha Mnazi Bay na kisima kimoja (1) katika eneo la Ntorya.

Shughuli hii ya uchorongaji visima inaendelea kwa eneo la Mnazi Bay ambapo kisima kimoja kati ya vitatu vitakavyochorongwa eneo hili kipo katika hatua za mwisho kukamilika.

Kukamilika kwa uchorongaji huu kunatarajiwa kuongeza uzalishaji wa gesi asilia kwa takribani futi za ujazo milioni 30 kwa siku kwa eneo la Mnazi Bay na futi za ujazo milioni 60 kwa siku kwa upande Ntorya. Kiasi hiki cha gesi asilia kama kitatumika kuzalisha umeme, basi kinaweza kuzalisha zaidi ya MW 400.

Aidha, hatua hii itaongeza upatikanaji wa nishati kwa matumizi ya uzalishaji wa umeme, viwandani, majumbani na usafiri.

Kufanyika kwa Tafiti za Msingi za Uwepo wa Mafuta na Gesi Asilia

PURA imesimamia uchukuaji wa data za mitetemo (seismic data) katika maeneo mapya yenye uwezekano wa kuwa na rasilimali za mafuta na gesi asilia.

Katika kipindi hiki jumla ya taarifa za mitetemo zenye eneo la kilomita za mraba (km2) zipatazo 265 zimechukuliwa. Shughuli hii ikijumuisha uchukuaji wa data za mitetemo za 3D za $km^2$ 185 katika maeneo ya Lindi na Mtwara na uchukuaji wa data za mitetemo za 2D kwa eneo la $km^2$ 80 katika eneo la Eyasi Wembere.

Tafiti hizi ni muhimu katika kutambua uwezekano wa upatikanaji wa rasilimali mpya za mafuta na gesi nchini.

Kuongeza Ushiriki wa Watanzania (Local Content) katika Shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli

Katika kipindi hiki, miradi ya mkondo wa juu wa petroli imezalisha ajira za moja kwa moja zaidi ya 110 kwa Watanzania kupitia miradi ya uchorongaji wa visima iliyopo kwenye hatua mbalimbali katika Kitalu cha Mnazi Bay na Eneo la Ntorya. Aidha, kampuni zaidi ya 12 za Kitanzania zimepata zabuni za kutoa huduma mbalimbali katika miradi hiyo.

Hatua hii inaendelea kuimarisha ushiriki wa wazawa katika sekta ya mafuta na gesi asilia na kuchochea maendeleo ya uchumi wa ndani.

Usimamizi Madhubuti wa Uzalishaji wa Gesi Asilia

PURA imeendelea kusimamia uzalishaji wa gesi asilia kutoka vitalu vya Mnazi Bay na Songo Songo.

Kwa sasa, uzalishaji wa gesi asilia nchini unafikia wastani wa futi za ujazo milioni 93 kwa siku, ambayo inatumika katika uzalishaji wa umeme, viwandani, kwa matumizi ya majumbani na nishati ya kuendeshea magari.

Kuanzishwa kwa Mfumo wa Kidigitali wa Usimamizi wa Gharama za Mikataba ya Utafutaji na Uzalishaji wa Gesi Asilia (PSA).

PURA imetengeneza mfumo wa unaojulikana kama Cost Recovery Management System (CRMS) unaotumika katika kaguzi za gharama zinazotumika na Makampuni ya utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa gesi asilia zilizokubaliwa kupitia mikataba ya PSA. Mfumo huu utasaidia kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa gharama za miradi ya mafuta na gesi na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa mikataba ya PSA.

Mfumo huu utafungamanishwa na mifumo mingine ya kiutendeaji na kiudhibiti kutoka Taasisi nyingine za Serikali.

**VIPAUMBELE VYA PURA**

Katika mwaka wa fedha 2025/2026, PURA inaendelea kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

Duru ya Tano ya Kunadi Vitalu vya Mafuta na Gesi Asilia

Serikali kupitia PURA inaendelea na maandalizi ya Duru ya Tano ya Kunadi Vitalu vya Utafutaji wa Mafuta na Gesi, ambayo inalenga kuvutia wawekezaji wapya, kuongeza uwekezaji katika sekta ya mafuta na gesi asilia na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Hatua hii itaongozwa na Mkataba Kifani wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (MPSA) utakaotumika katika mikataba mipya.

Maandalizi ya kusimamia Utekelezaji wa Mradi wa LNG

Serikali na wawekezaji katika vitalu vitatu vya bahari kuu ambavyo ni vitalu namba 1, 2 na 4 wanakamilisha majadiliano kuhusu utekelezaji wa mradi wa gesi asilia kuwa kimiminika (LNG Project) unaotarajiwa kuendelezwa kwa kutumia gesi asilia itakayozalishwa kutoka vitalu hivyo. Kukamilika kwa majadiliano haya na kuanza kwa utekelezaji wa mradi huu kutasaidia kuvutia uwekezaji mkubwa wa kimataifa, kuongeza ajira kwa Watanzania na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Kwa mujibu wa Sheria ya Petroli ya mwaka 2025, PURA ina jukumu la kusimamia na kudhibiti uwekezaji huo wa LNG. Ili kutekeleza wajibu huo kwa ufanisi, PURA imeendelea kufanya maandalizi ya kimkakati katika maeneo kadhaa muhimu ikiwemo, kushauri namna ya kuimarisha mfumo wa kisheria na Kanuni (Regulatory Framework); kujenga uwezo wa kitaasisi na rasilimali watu; kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini (monitoring and compliance); kuimarisha ushirikiano na taasisi nyingine za serikali na wadau; na kuimarisha usimamizi wa maslahi ya taifa na ushiriki wa wazawa (local content).

**HITIMISHO**

Kwa ujumla, mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki yanaonesha dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuendeleza sekta ya mafuta na gesi asilia kama kichocheo muhimu cha ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Kupitia usimamizi madhubuti wa shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa gesi asilia, pamoja na maandalizi ya miradi mikubwa ya kimkakati kama vile mradi wa LNG na Duru ya Tano ya kunadi vitalu vya utafutaji, PURA itaendelea kuhakikisha rasilimali za mafuta na gesi asilia zinasimamiwa kwa ufanisi, uwazi na kwa maslahi mapana ya Watanzania wa sasa na vizazi vijavyo.



# TIRA yafanikisha Bima ya Afya kwa Wote

Na Selemani Nzaro

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), inawahimiza Watanzania wote kushiriki kikamilifu katika mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kujiandikisha, kulipa michango stahiki na kuzingatia taratibu zilizowekwa.

Kutokana na maendeleo ya utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, TIRA inajivunia kufanikisha ahadi ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ndani ya Siku 100 kama alivyowaahidi Watanzania wakati wa kampeni za Uchaguzi wa Oktoba 29, 2025.

Ili kuimarisha huduma hiyo na kuwafanya wananchi kunufaika, TIRA inaendelea kutoa elimu kwa umma, kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote na kulinda haki za wanachama wa bima ya afya ili kuhakikisha utekelezaji wa bima ya afya unaboresha maisha na ustawi wa jamii.

Miongoni mwa majukumu ya TIRA katika kutekeleza bima ya afya kwa wote ni pamoja na kusajili vituo vya afya yaani kuanzia ngazi ya zahanati mpaka hospitali za rufaa. Kutokana na jukumu hilo, hadi sasa TIRA imefanikiwa kusajili watoa huduma 10,032 nchi nzima ambapo lengo ni kusajili watoa huduma 13,776 nchini kote.

Aidha, utekelezaji wa Sheria hiyo umekuwa ni sehemu ya maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 na mwaka 2025; na pia ni miongoni mwa vipaumbele vilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 vitakavyowezesha taifa kufikia uchumi wa kati.

TIRA yawezesha soko salama la bima.

Kamishna wa Bima Tanzania, Dk Baghayo Saqware anasema TIRA imeendelea kusimamia sekta ya bima kwa weledi na ufanisi hali iliyochangia sekta hiyo kukua kwa wastani wa asilimia 10 kwa kipindi cha miaka minne mfululizo.

Anasema mwaka 2024 mapato ya ada za bima yalifikia Sh. trilioni 1.52 ikilinganishwa na Sh. trilioni 1.24 mwaka 2023.

Sambamba na hayo, Dkt. Saqware anasema mchango wa sekta ya bima katika Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 2.01 mwaka 2023 hadi asilimia 2.08 mwaka 2024.

### *Sekta ya bima inavyoimarisha uchumi wa taifa*

Sekta ya bima ni miongoni mwa sekta muhimu zinazochangia kwa kiasi kikubwa ukuaji na ustahimilivu wa uchumi wa Taifa kupitia ulinzi wa mali na shughuli za kiuchumi kwa wananchi pamoja na taasisi za umma na binafsi.

Hoja hiyo inathibitishwa na Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar ambaye anasema hilo linawezekana kwa taasisi za umma na binafsi kupata fidia ikiwemo gharama za matibabu pindi majanga ya mali au ugonjwa yanapotokea.

Balozi Dkt. Khamis anaipongeza TIRA kwa kusimamia soko la bima kwa weledi, kutoa elimu kwa umma na kulinda haki za wananchi huku akisisitiza umuhimu wa Bima ya Afya kwa Wote katika kupunguza athari za kifedha kwa wananchi.

"Ukataji wa bima huongeza imani ya wawekezaji, hulinda rasilimali za serikali na sekta binafsi na hupunguza Athari za kifedha kwa wananchi wakati wa majanga," anasema Balozi Dkt. Khamis wakati wa kikao kati yake na ujumbe wa TIRA ukiongozwa na Dkt. Saqware hivi karibuni.



*Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan*
*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

### *TIRA yainadi Bima ya Afya kwa Wote hadi wilayani*

Juhudi za TIRA kuinadi kwa wananchi Bima ya Afya kwa Wote zimeendelea katika mikoa na wilaya mbalimbali hapa nchini kwa lengo la kutoa elimu kwa wadau na wananchi juu ya umuhimu na faida za kujiunga na huduma hiyo hapa nchini kupitia programu ya wilaya kwa wilaya.

Katika kulitekeleza hilo, TIRA imegawa nchi katika kanda 10 ili iwe rahisi kuwafikia wananchi wote waweze kupata huduma hiyo muhimu kwa afya na maisha yao pamoja na vizazi vijavyo.

Kanda hizo na mikoa yake katika mabano ni Kanda ya Kaskazini (K'njaro, Arusha,Tanga), Kanda ya Mashariki (Morogoro, Pwani, Dar), Kanda ya Kusini (Mtwara, Lindi, Ruvuma), Nyanda za Juu Kusini (Songwe, Njombe, Mbeya) na Kanda ya Kati (Iringa, Dodoma, Manyara).

Kanda nyingine ni Kanda ya Ziwa (Geita, Mwanza, Kagera, Mara, Simiyu), Kanda ya Tanganyika (Kigoma, Katavi, Rukwa), Kanda ya Magharibi (Shinyanga, Tabora, Singida), Kanda ya Pemba (Pemba Kusini, Pemba Kaskazini) na Kanda ya Unguja (Unguja Kaskazini, Unguja Kusini na Unguja Magharibi).

### *TIRA yavalia njuga udanganyifu sekta ya bima*

Katika kupambana na udanganyifu sekta ya bima, TIRA inaendelea kutoa mafunzo maalum kwa maofisa madai na maofisa sheria wa kampuni za bima nchini kwa lengo la kuwajengea uelewa kuhusu hali ya udanganyifu katika bima, Athari zake pamoja na mbinu za kuzuia na kudhibiti vitendo hivyo.

Kamishna wa Bima nchini, Dkt. Saqware anasema TIRA imebaini kuwepo kwa vitendo mbalimbali vya udanganyifu katika sekta ya bima hali iliyosababisha kuanzishwa kwa kitengo cha udhibiti wa udanganyifu kuhakikisha soko la bima linaendelea kuwa imara na la kuaminika.

### *Kuimarisha uwajibikaji kupitia e-Mrejesho*

Kadhalika, TIRA imeendelea kutoa mafunzo ya matumizi ya mfumo wa e-Mrejesho kwa watumishi wake kwa lengo la kuboresha uwazi, uwajibikaji na mawasiliano kati ya taasisi na wananchi.



*Dkt. Baghayo Abdallah Saqware*
*Kamishna wa Bima*

Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Nakaunda Mangosongo anasema matumizi stahili ya mfumo huo yatawezesha maoni, mapendekezo na malalamiko ya wananchi kuhusu huduma za bima yanapatiwa majibu kwa wakati na kwa ufanisi.

### *Utekelezaji sheria ya Bima ya Afya kwa Wote*

Katika utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, TIRA imechukua hatua mbalimbali kwenye utekelezaji ikiwa ni pamoja na kuboresha mifumo ya Tehama kama vile ya usajili wa watoa huduma za bima ikiwemo vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Pia, imeboresha mfumo wa usimamizi wa watoa huduma za bima katika soko la bima na mfumo wa kuwezesha ufanyaji biashara ya bima katika soko la bima.

Katika eneo la Tehama, TIRA imeunganishwa na mifumo ya taasisi nyingine zikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), Jeshi la Polisi, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)

### *Kupokea na Kushughulikia Malalamiko.*

Meneja Uhusiano na Mawasiliano TIRA, Hadija Maulid anasema ili kuhakikisha wateja na wanufaika wa bima wanapata huduma bora za bima kwa mujibu wa Sheria na Kanuni, TIRA imeandaa miongozo ya kupokea na kushughulikia malalamiko yanayohusu madai na utoaji wa huduma za bima.

Anasema TIRA imeainisha utaratibu wa kupokea malalamiko kutoka kwa wadau wa bima kwa lengo la kutatua changamoto wakati wa utoaji wa huduma za bima za afya.

Anataja aina za malalamiko yanayoshughulikiwa kuwa ni mnufaika kutoridhishwa na huduma alizopatiwa na mtoa huduma, mnufaika kutopatiwa huduma kwa mujibu wa mkataba wa bima, mnufaika kuwekewa vipengele visivyotekelezeka katika mkataba wa bima, mnufaika au mtoa huduma kutoridhika na kiwango cha madai kilicholipwa na mnufaika au mtoa huduma kucheleweshwa kulipwa madai ya bima.







# SIKU 100 ZA RAIS DKT SAMIA SULUHU HASSAN

## WIZARA YA ARDHI YAPANGA NA KUPIMA EKARI 85,517.5 TAYARI KWA UWEKEZAJI WA VIWANDA NA UKUAJI WA UCHUMI NCHINI



*Dhana ya kupanga na kupima ardhi*

**Na Munir Shemweta, WANMM, Dodoma**

SIKU 100 za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tangu aapishwe kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Novemba 3, 2025 Dodoma, zinathibitisha dhamira yake ya kuimarisha uchumi wa nchi kupitia uwekezaji wa kimkakati.

Moja ya hatua muhimu zilizochukuliwa ni kutengwa ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda na shughuli za kiuchumi, hatua inayolenga kuchochea ukuaji wa sekta ya uzalishaji, kuongeza ajira na kuinua maisha ya Watanzania.

Rasilimali ardhi ni fursa muhimu kwa ukuaji wa Uchumi wa Taifa na kuwaletea wananchi maendeleo ya endelevu kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

"Mheshimiwa Rais amekuwa akisisitiza kuwa Serikali yake itahakikisha kazi zinafanyika kwa kuzingatia misingi ya utu katika kukuza uchumi na kipato cha wananchi pamoja na

kudumisha demokrasia na utawala," anasema Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Dkt. Leonard Akwilapo.

Kwa kuzingatia kuwa Ardhi ni rasilimali muhimu inayotoa fursa kwa ajili ya maendeleo ya kilimo, viwanda, makazi na shughuli nyingine za kiuchumi, Tanzania ina takriban




*Kamati ya Kitaifa ya Kugawa Ardhi imetembelea kiwanda cha mbegu cha Seed Co Tanzania Limited na kujionea kasi ya ujenzi, huku Operesheni Meneja wa Kiwanda Bw:Andrew Ngowi ikieleza mipango na mikakati ya utekelezaji wa mradi huo unaotarajiwa kuongeza uzalishaji wa mbegu bora, ajira kwa wananchi na kuchochea maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.*



*Vifaa vya kupima ardhi*

kilomita za mraba 883,600 za Ardhi ambayo ni muhimu kwa maendeleo endelevu.

Dira ya Taifa ya Maendeleo (Dira 2050), inaweka mkazo wa kisera kuimarisha usimamizi bora ili kuvutia uwekezaji unaotegemea ardhi. Hatua hiyo inasaidia kuwa na iliyopangwa vizuri na kuweka wazi matumizi ya ardhi yakiwemo maeneo ya viwanda.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikiongozwa na maono ya Serikali ya

Awamu ya Sita, imefanikiwa kupanga na kupima ardhi tayari kwa wawekezaji, ikiwa ni

ishara ya utekelezaji wa vitendo wa maono hayo ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan,

katika kujenga uchumi shindani na endelevu.

Aidha, Wizara imehakiki ardhi iliyoainishwa kwenye Mipango Kabambe, Mipango Kina

na Mipango ya Maeneo Maalumu ya Kiuchumi katika mikoa 26 na kubaini ardhi yenye

ukubwa wa ekari 360,462.5 kutengwa kwa ajili ya matumizi ya viwanda.

Kupitia maono hayo ya Mheshimiwa Rais, wizara imefanikiwa kupanga na kupima jumla ya ekari 85,517.5 ambazo sasa ziko tayari kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda na nah atua za kutafuta maeneo mengine zikifanyika kuzifikia wilaya zote nchini.

Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda yapo katika halmashauri mbalimbali nchini katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kigoma, Lindi, Morogoro, Pwani pamoja na mkoa wa Ruvuma.

Katika mkoa wa Kigoma, maeneo yaliyotengwa yapo katika halmashauri ya wilaya ya Kibondo, eneo la Kibondo lenye ukubwa wa ekari 17,836.11 na halmashauri ya wilaya ya Uvinza DC katika maeneo ya Basanza ekari 19,908.89 na Lugufu ekari 26,910.25.

Mkoa wa Dodoma ni katika halmashauri ya wilaya ya Kondoa, eneo la Pahi lenye jumla ya ekari 20; halmashauri ya wilaya ya Kongwa, eneo la Sejeli lenye ukubwa wa ekari 200.00 na Mbande ekari 9,884.21.

Ruvuma, maeneo yaliyotengwa yapo katika manispaa ya Songea, eneo la Mwengemshindo ekari 5,000.00 pamoja na Madaba, eneo la Magingo lenye ukubwa wa ekari 129.50.



*Wafanyakazi wakiendelea na shughuli za uzalishaji wa nguo katika Kiwanda cha Took Garmet kilichopo Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA), Ubungo External*

Kwa upande wa mkoa wa Lindi, eneo la uwekezaji lipo manispaa ya Lindi katika eneo la Ngongo ekari 11.14, Kikwetu ekari 46.19 na eneo la Ngurumahamba lenye ukubwa wa ekari 49.23.

Mkoa wa Arusha umetengewa eneo katika halmashauri ya wilaya ya Meru eneo la Tanzania Plantation lenye ukubwa wa ekari 1,000.00 wakati mkoa wa Tabora eneo lililotengwa ni Kalunde katika manispaa ya Tabora ekari 250.00.

Dar es Salaam, katika manispaa ya Kigamboni zimetengwa ekari 900.00 katika eneo la Pembamnazi. Mkoa wa Morogoro umetengewa ekari 2,000.00 katika eneo la Shamba la Manji katika halmashauri ya wilaya ya Mvomero pamoja na halmashauri ya wilaya

ya Kilosa, eneo la Kimamba, ekari 672.00 wakati mkoa wa Pwani, katika halmashauri

ya wilaya ya Kibaha, zimetengwa ekari 700.00 katika eneo la Kikongo.

"Ardhi hii ya uwekezaji ina faida kubwa, inatoa ajira kwa wananchi wa maeneo husika

kutokana na uwekezaji, miundombinu na huduma za jamii inaboreshwa, thamani ya

ardhi ya wananchi iliyopakana na maeneo ya uwekezaji inaongezeka na kuchochea

maendeleo ya kiuchumi," anasema Mheshimiwa Dkt. Akwilapo.

Hatua ya Serikali ya kutenga, kupanga na kupima ardhi kwa ajili ya uwekezaji ndani ya

siku 100 za awamu ya pili ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni ushahidi wa uongozi

thabiti unaojikita katika vitendo na matokeo. Mafanikio haya yanaweka msingi imara wa

kuvutia wawekezaji wa ndani na nje yanasaidia kuharakisha maendeleo ya viwanda na kukuza uchumi wa taifa kwa njia endelevu.

Kwa msingi huo, maendeleo ya wananchi yanabaki kuwa kipaumbele cha juu cha Taifa,

huku ardhi ikiendelea kuwa rasilimali muhimu ya kuendesha ajenda ya Tanzania ya

uchumi wa viwanda na ustawi wa watu wake kwa kuzingatia tunu za Taifa ambazo ni

utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi na uwajibikaji.



*Wafanyakazi wakiunganisha magari katika Kiwanda cha kuunganisha malori na matipa cha Saturn Corporation Limited kilichopo wilaya ya Kigamboni*



# Siku 100 za hatua madhubuti za Dkt. Samia sekta ya ujenzi – Kazi na Utu Tunasonga Mbele

*Ujenzi wa Daraja la Pangani lenye urefu wa mita 525 na Barabara unganishi zenye urefu wa Kilomita 25 ukiendelea.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa Daraja la Mto Pangani lenye urefu wa mita 525 mkoani Tanga.*

KATIKA safari ya maendeleo ya taifa lolote, miundombinu ya barabara na madaraja huwa ni nguzo muhimu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Kutokana na umuhimu wake huo, ndani ya siku 100 za uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kupitia falsafa yake ya 'Kazi na Utu Tunasonga Mbele' ameipa kipaumbele sekta ya ujenzi akilenga kuchochea maendeleo ya wananchi wake na Taifa kwa ujumla.

Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, inasimamia ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara, madaraja, majengo ya serikali, vivuko, mitambo na magari ya serikali na uendeshaji wa vivuko, ikilenga upatikanaji wa miundombinu bora, salama na endelevu na inayochochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

Wizara pia inasimamia na kudhibiti ubora na usalama wa kazi zote za ujenzi wa barabara, madaraja, vivuko, majengo, mitambo, mifumo ya umeme na vifaa vya kielektroniki, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali huku ikizingatia thamani ya fedha.

Kwa kulitambua hilo, serikali imeendelea kuweka misingi imara ya kuhakikisha sekta ya ujenzi inakuwa chachu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa Watanzania kwa kuzingatia misingi ya usawa, ushirikishwaji na uzalendo wa kiuchumi.

Katika siku 100 za uongozi wa Rais Samia, serikali imeonesha kwa vitendo falsafa ya Kazi na Utu kwa kuhakikisha miradi ya maendeleo ya sekta ya ujenzi, inatekelezwa kwa kasi na uwazi ikilenga kumnufaisha mwananchi.

Kutokana na kasi ya utoaji rasilimali fedha kwa wakati kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya sekta ya ujenzi, kumeifanya Wizara ya Ujenzi kuwa na ufanisi na uendelevu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati.

Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega anasema ndani ya siku 100 za uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, wizara kupitia Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS), imekamilisha ujenzi wa miradi 40 kati ya miradi 81 ya madaraja ya dharura inayotekelezwa chini ya programu maalumu ya Contingent Emergency Response Component (CERC), inayofadhiliwa na Benki ya Dunia yenye thamani ya Shilingi bilioni 500 ambapo utekelezaji wa miradi hiyo umekwenda kutatua changamoto na kuleta tabasamu kwa wananchi.

Miradi ya madaraja ya dharura iliyokamilika ni Daraja la King'ori (Arusha), Msimbagenge (Pwani), Morena (Dodoma), Fufu (Dodoma), Nzali (Dodoma), Kamishango (Kagera), Katuma (Katavi), Washi (Hedaru - Kilimanjaro).

Mingine ni Daraja la Kipwata (Lindi),

Mikereng'ende (Lindi), Matandu (Lindi), Somanga Mtama (Lindi), Katesh (Manyara), Losinyai (Manyara), Minjingu (Mulungu - Manyara na Chakwale (Morogoro).

Miradi hiyo ilianzishwa kufuatia athari za mvua za El Niño na Kimbunga Hidaya kati ya Oktoba, 2023 hadi Mei, 2024 ambapo miundombinu ya barabara na madaraja iliathirika katika mikoa mbalimbali ikiwamo Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Lindi, Rukwa, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mwanza, Manyara, Geita, Kagera, Shinyanga, Simiyu na Mara.

Aidha, Ulega anasema katika kuimarisha mtandao wa barabara, serikali imesaini mkataba na Benki ya Dunia kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Makambako–Songea kwa kiwango cha lami, ikijumuisha Rutukila – Songea na Songea Bypass zenye urefu wa kilometa 95.1 kwa gharama ya Shilingi bilioni 158.67.

"Taratibu za kuanza kazi za ujenzi kwa mradi huu zinaendelea na kukamilika kwake kunatarajia kufungua fursa mpya za kiuchumi Kusini mwa Tanzania," anasema Ulega.

Sambamba na utekelezaji wa miradi hiyo, Wizara ya Ujenzi imepokea kiasi cha Shilingi bilioni 511.36 kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi wa miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja nchini ambapo fedha hizo zinajumuisha fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha Shilingi bilioni 284.83 na Shilingi bilioni 226.53 kutoka wa wadau wa maendeleo.

Katika kuwezesha ushirikishwaji wa wanawake na vijana katika sekta ya ujenzi, Ulega anasema serikali imezipatia kampuni nne za wakandarasi wanawake wa ndani mradi maalumu wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ruanda – Idiwili yenye urefu wa kilometa 20 mkoani Songwe.

"Utekelezaji wa mradi huo unaendelea na umefikia asilimia 10.4 na katika kipindi cha siku 100 za uongozi wa Rais Samia madarakani tayari makandarasi hao wamelipwa malipo ya awali yenye jumla ya Shilingi bilioni 6.87," amebainisha Ulega.

Aidha, Wizara ya Ujenzi kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) imewawezesha vijana na wanawake kupitia mafunzo kwa vitendo katika miradi mikubwa ya kitaifa na kimataifa hatua inayojenga kizazi kipya cha wataalamu wa ujenzi.

Kupitia programu hiyo, wahandisi wahitimu watano wamepata mafunzo katika mradi wa kimataifa wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Rumonge – Gitaza na Kabingo – Kasulu – Manyovu.

Pia kupitia mradi wa kudhamini wanawake kwa kushirikiana na Ubalozi wa Norway, jumla ya wahandisi wahitimu wanawake 147 wamepata nafasi za mafunzo kwa vitendo katika taasisi za umma na binafsi.

Ulega anasema ndani ya siku 100 za uongozi wa Rais Samia, wahitimu 289 katika fani ya ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi wanaendelea kupatiwa mafunzo ya vitendo kupitia programu ya Archicture and Quantity Survey Internship Programme (AQIP) inayoratibiwa na Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB).

Aidha, Ulega anasema katika siku 100 za uongozi wa Rais Samia, serikali kupitia Wakala ya Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA), imetoa jumla ya Shilingi bilioni 10.278 kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa vivuko vya MV Magogoni na MV Kigamboni ambapo ukarabati huo unaendelea.

Ulega anasema ndani ya siku 100 za uongozi wa Rais Samia, serikali imetoa bilioni 20 kwa Wakala ya Tanzania (TBA) kwa ajili ya kazi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa nyumba 150 kwa ajili ya makazi ya watumishi wa umma awamu ya pili katika eneo la Nzuguni jijini Dodoma ambapo ujenzi unaendelea na umefikia asilimia 34.

Kazi zingine ambazo zimefanyika ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa majengo mawili ya ghorofa (Block C & D) yenye uwezo wa kuchukua familia 32 katika eneo la Magomeni Kota ambao umefikia asilimia 78.

Pia kuendelea na ujenzi wa jengo moja la ghorofa lenye uwezo wa kuchukua familia 14 katika eneo la Ghana Kota jijini Mwanza uliofikia asilimia 39.

Wakala pia umeendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa majengo mawili ya ghorofa ya makazi katika eneo la Canadian Village - Masaki jijini Dar es Salaam ambao uko asilimia 95.

Kwa hakika, siku 100 za uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan zimeacha alama inayoonekana katika sekta ya ujenzi, ni siku 100 za vitendo, uwajibikaji na kuzingatia utu wa mwananchi.

Kupitia miradi ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa nchini, serikali imeendelea kuimarisha miundombinu na kufungua fursa mpya za kiuchumi na kijamii ambapo juhudi hizi zinajenga msingi imara wa maendeleo endelevu ambapo manufaa yake yanamgusa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.





# Tarura: Nguzo ya kimkakati ya uchumi wa wananchi katika uongozi wa Awamu ya Sita

**Na Catherine Sungura**

NDANI ya siku 100 za mwanzo wa Uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali ya Awamu ya Sita iliweka wazi dira yake ya uongozi unaotanguliza vitendo, maamuzi ya haraka na majibu yanayogusa maisha halisi ya wananchi. Miongoni mwa maeneo yaliyopewa msukumo wa kimkakati katika kipindi hicho ni sekta ya barabara za vijijini na mijini, sekta ambayo ndiyo mhimili wa uchumi wa wananchi walio wengi.


Barabara si miundombinu ya kawaida ni uti wa mgongo wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Ndizo zinazounganisha mkulima na soko, mfanyabiashara na mteja, mwanafunzi na shule, mgonjwa na kituo cha afya. Kwa kulitambua hilo, Rais Samia alitoa maelekezo ya wazi kwamba barabara zinazogusa maisha ya wananchi wa kawaida zipatiwe kipaumbele cha juu katika upangaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Maelekezo hayo yaliweka msingi wa mageuzi makubwa yaliyokuja kutekelezwa kupitia Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), taasisi iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. TARURA inasimamia mtandao wa barabara za Wilaya wenye urefu wa kilomita 144,149.18, mtandao unaobeba sehemu kubwa ya shughuli za uzalishaji na mzunguko wa uchumi wa ndani.

Ndani ya siku 100 za mwanzo wa Rais Samia, mwelekeo mpya wa utekelezaji ulionekana wazi, fedha kuelekezwa moja kwa moja kwenye miradi, vikwazo vya kiutawala kupunguzwa, na wananchi kuanza kuona matokeo katika maeneo yao. Hii ilirejesha imani ya wananchi kuwa barabara za vijijini na mijini hazipo pembezoni mwa ajenda ya maendeleo ya Taifa.

Msingi huo wa awali umejidhihirisha baadaye kupitia uamuzi mkubwa wa Serikali ya Awamu ya Sita kuongeza bajeti ya taasisi hii kutoka shilingi bilioni 275 mwaka 2021/22 hadi shilingi bilioni 944.11 mwaka 2025/26, sawa na ongezeko la asilimia 243. Hatua hii ilidhihirisha kwa vitendo kuwa maelekezo ya Rais Samia yaliambatana na rasilimali na dhamira ya utekelezaji.

Matokeo ya msukumo huo wa kimkakati yanaonekana wazi katika hali ya mtandao wa barabara za wilaya. Hivi sasa barabara zilizo katika hali nzuri na wastani zimefikia asilimia 66.31, sawa na kilomita 95,779.76, ikilinganishwa na asilimia 52.07 mwaka 2021. Haya ni mafanikio yanayoakisi uongozi unaoanza kwa dira sahihi na kuendelezwa kwa uthabiti.




Utafiti uliofanywa na TARURA kwa kushirikiana na Economic and Social Research Foundation (ESRF) unaonesha wazi mchango wa barabara katika kuchochea uchumi wa wananchi. Upitikaji wa barabara za vijijini umefikia asilimia 74, huku upatikanaji wa usafiri katika barabara zilizoboreshwa ukiwa asilimia 86, ikilinganishwa na asilimia 20 pekee kwa barabara ambazo hazijaboreshwa. Hii ni ishara tosha kuwa uwekezaji kwenye barabara ni uwekezaji wa moja kwa moja kwenye ustawi wa wananchi.

## Kupungua kwa Gharama za Usafirishaji wa Mazao

Kupungua kwa muda na gharama za usafiri ni ushahidi mwingine wa wajibu wa kimkakati wa TARURA katika uchumi. Muda wa kufika masokoni umepungua kwa asilimia 43.6, gharama za usafiri na usafirishaji zimepungua kwa asilimia 75.3, na wananchi sasa wanafikia huduma za kifedha na kijamii kwa urahisi zaidi. Hali hii imeongeza tija ya uzalishaji, mzunguko wa fedha na kipato cha kaya nyingi za vijijini.

Uboreshaji wa barabara kupitia TARURA umeleta mabadiliko makubwa katika sekta ya kilimo na biashara ya mazao. Kabla ya ujenzi wa barabara, wakulima wengi walilazimika kutumia gharama kubwa kusafirisha mazao yao kutokana na ubovu wa miundombinu. Hali hii ilipunguza faida na wakati mwingine kusababisha

mazao kuharibika njiani. Kupitia barabara mpya na zilizokarabatiwa, gharama za usafirishaji zimepungua kwa kiwango kikubwa, hali inayowawezesha wakulima kufikisha mazao sokoni kwa haraka na kwa gharama nafuu. Matokeo yake, wakulima wameongeza mapato yao na kupata motisha ya kuongeza uzalishaji.

## Kupungua kwa Upotevu wa Mazao na Kuongezeka kwa Kipato cha Wakulima

Katika sekta ya kilimo ambayo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa, uboreshaji wa barabara umeleta mabadiliko makubwa katika mnyororo mzima wa uzalishaji na masoko ya mazao. Barabara bora zimepunguza kwa kiasi kikubwa ucheleweshaji wa usafirishaji wa mazao kutoka mashambani hadi masokoni na viwandani hali iliyosababisha upotevu wa mazao kupungua kwa asilimia 72.5.

Kwa mfano, katika zao la chai, zaidi ya asilimia 54.3 ya uzalishaji ilikuwa ikipotea awali kutokana na mazao kuchelewa kufikishwa viwandani au kuharibika njiani kwa sababu ya ubovu wa barabara. Kupitia maboresho yaliyofanyika wakulima sasa wanafikia masoko kwa wakati, ubora wa mazao unaendelea kuhifadhiwa na gharama za usafirishaji zimepungua kwa kiasi kikubwa.

## Ajira kwa Vijana kupitia miradi ya barabara

Mojawapo ya manufaa makubwa ya miradi ya TARURA ni upatikanaji wa ajira kwa vijana. Katika hatua za ujenzi na matengenezo ya barabara yaliyofanywa katika miradi iliyosimamiwa na TARURA jumla ya ajira 11,316 zilitolewa katika kipindi cha miezi (6) kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Ajira hizo zinajumuisha wanawake na vijana kama mafundi, vibarua, waendeshaji wa mitambo pamoja na wasaidizi wa kazi mbalimbali. Ajira hizi ingawa baadhi ni za muda lakini zimekuwa chanzo muhimu cha kipato kwa vijana wengi waliokuwa hawana ajira rasmi. Kwa baadhi ya miradi vijana waliopata ujuzi wa kazi za ujenzi wameendelea kupata ajira za kudumu au kujiajiri katika shughuli zinazohusiana na ujenzi na matengenezo ya miundombinu. Hali hii imepunguza tatizo la ukosefu wa ajira na kuongeza mchango wa vijana katika maendeleo ya kiuchumi.

## Ongezeko la Kipato cha Kaya na Kupungua kwa Umaskini

Kwa ujumla miradi ya TARURA imechangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa kipato cha kaya katika maeneo mengi ya vijijini. Kupitia ajira, kupungua kwa gharama za usafirishaji na wananchi wameweza kuboresha hali zao za kiuchumi. Ongezeko la kipato limewasaidia wananchi kugharamia mahitaji ya msingi kama elimu, afya na chakula bora. Hatua hii imekuwa muhimu katika kupunguza umaskini na kuongeza uwezo wa wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kuchangia pato la taifa.

## Huduma za Afya

Miundombinu ya barabara iliyoboreshwa imekuwa chachu ya kuboresha upatikanaji wa huduma za afya. Wagonjwa sasa wanaweza kufika katika vituo vya afya, zahanati na hospitali kwa wakati, hata katika hali za dharura. Vilevile, usafirishaji wa dawa, vifaa tiba na wataalamu wa afya umeboreshwa, hivyo kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma. Kwa ujumla, ujenzi wa barabara kupitia TARURA umechangia kupunguza vifo vinavyotokana na ucheleweshaji wa matibabu, hasa kwa wajawazito na watoto.

## Huduma za Shule

Sekta ya elimu imepata manufaa makubwa kutokana na uboreshaji wa miundombinu ya barabara. Wanafunzi wamepata urahisi wa kufika shuleni bila vikwazo, jambo lililoongeza mahudhurio na kupunguza utoro. Barabara bora zimewasaidia walimu kufika shule za vijijini kwa urahisi, hali iliyoongeza morali na kuboresha ubora wa ufundishaji. Pia, usafirishaji wa vifaa vya elimu na miundombinu ya shule umefanyika kwa ufanisi zaidi, hivyo kuchangia mazingira bora ya kujifunzia.



## Usalama Barabarani na Miundombinu Himilivu kwa Mabadiliko ya Tabianchi

Masuala ya usalama barabarani na mabadiliko ya tabianchi nayo yamezingatiwa kikamilifu. Uwezekano wa ajali katika barabara zilizoboreshwa ni asilimia 14 ikilinganishwa na asilimia 20 kwa barabara ambazo hazijaboreshwa. Aidha, athari za mafuriko na mmomonyoko wa udongo zimepungua kwa kiasi kikubwa, matokeo ya ujenzi wa miundombinu himilivu unaozingatia mazingira moja ya maelekezo ya msingi ya Rais Samia tangu mwanzo wa uongozi wake.

Hivyo Wakala inahakikisha barabara zote zinazojengwa zinafanyiwa usanifu na kuhakikisha zinafikia hadhi ya Nyota tatu (3) au zaidi. Miundombinu kama vile maeneo ya waenda kwa miguu, alama za barabarani, taa za barabarani na vivuko vinazingatiwa hii yote katika kuhakikisha barabara zinakuwa salama kwa watumiaji.

Kwa mujibu utafiti wa upitikaji wa barabara za vijijini (Rural Accessibility Index (RAI)) uliofanywa na TARURA mwaka 2025 umeonesha kuwa, ufikiwaji wa mtandao wa barabara za vijijini, Tanzania Bara umefikia asilimia 61.0, kutoka asilimia 24.6 mwaka 2016 kwa utafiti uliofanywa na bank ya dunia (WB). Ongezeko hili linaonesha mchango mkubwa wa serikali ya Awamu ya Sita katika kuhakikisha TANROADS na TARURA zinaboresha mtandao wa Barabara za vijijini ili kufungua fursa za kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa maeneo ya vijijini.

Kwa ujumla, siku 100 za mwanzo wa uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan zimekuwa mwanzo wa safari ya mageuzi yenye mwelekeo wa wananchi. Kupitia TARURA, Serikali ya Awamu ya Sita imeonesha kuwa barabara si miundombinu tu, bali ni injini ya uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla.



# Wizara ya Katiba na Sheria inavyowavusha wanawake kutoka kwenye changamoto za kisheria hadi ushindi

*Mkurugenzi wa Huduma za Msaada wa Kisheria Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Ester Msambazi (Kushoto) akitoa huduma hiyo kwa wananchi wa mkoa wa Tanga wakati wa utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, Aprili 08, 2025 Jijini hapo.*

KATIKA mapambazuko ya kila siku, kuna sauti ya upole lakini yenye mamlaka inayoliamsha Taifa, ni sauti ya mama anayemwandaa mwanae kwenda shule, ni sauti ya kiongozi anayetoa maelekezo ya kiserikali, ni sauti ya mkulima anayepalilia mustakabali wa chakula nchini, ni jitihada za binti mdogo pale gengeni akiwa anapanga nyanya kusubiri wateja ili ajiendeleze kielimu.

Mwezi Machi ni mwezi maalum kwa wanawake duniani kote. Ni wakati wa kuangalia nyuma na kuona umbali tuliofika, ni wakati wa kuangalia mbele na kuona changamoto zilizopo katika harakati za kufikia usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake. Katika muktadha huu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, inajivunia kuwasilisha mchango wake katika kuwawezesha wanawake kupitia utoaji wa huduma za Msaada wa Kisheria zinazolenga kulinda na kutetea haki zao.

Kwa mujibu wa Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, usawa mbele ya sheria na haki ya kupata haki ni haki ya kila raia. Hata hivyo, utafiti na uzoefu umeonesha kuwa wanawake, hasa wale waishio vijijini na wenye kipato cha chini, wamekuwa wakikabiliwa na vikwazo vingi katika kupata haki zao. Vikwazo hivi ni pamoja na umasikini, ukosefu wa elimu ya sheria, mila potofu, na umbali mrefu wa Mahakama.

Ni kutokana na hali hiyo ambapo Wizara ya Katiba na Sheria imeendelea kutekeleza dira ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, inayojikita katika falsafa ya 4R za Upatanisho, Ustahimilivu, Marekebisho na Kujenga Upya, kwa kuhakikisha huduma za msaada wa kisheria zinawafikia wananchi wote, hasa wanawake na makundi maalum kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (MSLAC).

Kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), hasa Lengo la 5 la Usawa wa Kijinsia na Lengo la 16 la Amani na Haki zinaweka msisitizo mkubwa katika nguzo ya Utawala bora, Haki, Usawa Mbele ya sheria na inatoa mwanga jinsi huduma za kisheria zinavyoweza kuchangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Mifumo hii ya kimkakati ya maendeleo inatoa mwelekeo wa utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kama sehemu ya utekelezaji wake wa kutimiza haki kwa makundi yote hasa wenye uhitaji mkubwa wakiwemo wanawake.

## Jinsi Wizara ya Katiba na Sheria inavyowavusha wanawake kutoka kwenye changamoto hadi ushindi

Wizara ya Katiba na Sheria, kwa mujibu wa Sheria ya Msaada wa Kisheria (Sura ya 21), ina jukumu la msingi la kuratibu, kusimamia na kutoa huduma za msaada wa kisheria nchini. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara imeweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha wanawake wanaifikia haki kupitia huduma za msaada wa kisheria stahiki kwa wakati na kwa urahisi.

## Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia

Huduma za Msaada wa kisheria zimekuwa daraja muhimu linalowawezesha wanawake kutoka kwenye changamoto za kisheria. Wizara imewezesha uwepo wa Mashirika yanayotoa huduma za Msaada wa Kisheria kwa kusajili mashirika 284 ngazi za kijamii. Wizara imefanya mafunzo na kusajili Wasaidizi wa Kisheria 1,844 wanaofanya kazi katika Kata 3,314 nchi nzima. Aidha, Wizara kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (MSLAC) na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imefanikiwa kuwatembelea wanawake katika maeneo mbalimbali kutoa huduma jumuishi za kisheria ikiwemo kuwaelimisha kuhusu haki na wajibu wao, kutatua changamoto zao za kisheria ikiwemo masuala ya mirathi, ndoa, migogoro ya ardhi, matunzo ya Watoto ambayo suluhu za changamoto hizo zilimpatia mwanamke ushindi. Wanawake pia walipata huduma ya kupata usajili wa matukio muhimu ikiwemo vyeti vya kuzaliwa,vyeti vya vifo vya wapendwa wao ili waweze kushughulikia masuala ya mirathi.

Kupitia Kampeni hiyo jumla ya wananchi 4,157,065 walionufaika na huduma za Msaada wa Kisheria, wanawake walikuwa ni 2,135,902 na wanaume 2,021,163, jambo linaloashiria wanawake wengi kuwa ni miongoni mwa

makundi yenye uhitaji mkubwa wa huduma za kisheria na ni makundi yaliyonufaika zaidi kupitia Kampeni hiyo.

Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Campaign) chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ni jitihada kubwa ya kitaifa yenye lengo la kupanua wigo wa upatikanaji wa haki, kulinda haki za wanawake, kupambana na ukatili wa kijinsia (GBV), na kujenga mfumo wa haki wa usawa ambao haumuachi mwanamke wala msichana yeyote nyuma.

Uanzishwaji wa Madawati ya Msaada wa Kisheria. Wizara imefanikiwa kuanzisha Madawati ya Msaada wa Kisheria katika Halmashauri zote 184 za Tanzania Bara. Madawati haya ni kituo cha kudumu cha wananchi, wakiwemo wanawake, kupata ushauri wa kisheria, ushauri nasaha, upatanishi, na maelekezo ya kisheria karibu na maeneo yao ya makazi. Hii imepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za kusafiri hadi mahakamani na kuwafanya wanawake kuwa na ujasiri wa kufika na kusema shida zao ili zipate suluhu. Kupitia uanzishwaji wa Madawati ya Msaada wa Kisheria katika Halmashauri zote, Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, ushirikiano na wadau mbalimbali, na matumizi ya teknolojia, Wizara imeweza kuvunja vizuizi vya kijiografia na kifedha vilivyowatenga wanawake kuweza kufikia haki zao.

Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala (ADR). Watoa huduma walifanikiwa kusuluhisha migogoro 91,950 kwa kutumia njia mbadala. Katika suluhu hizi, wanawake waliongoza kwa asilimia 57.4, ikilinganishwa na wanaume waliofikia asilimia 42.6. Hii inaashiria uwezo wao wa mawasiliano, uvumilivu, utayari wa kushirikiana na kuweka mbele maslahi mapana ya familia au jamii. Kupitia mbinu hizi, wameweza kukamilisha migogoro yao kwa amani, kulinda mahusiano na muda unaotumika katika taratibu za Mahakama.

## Utoaji wa elimu ya uraia na utawala bora

Wizara kwa kutambua umuhimu wa elimu katika kuijenga jamii imetoa mafunzo ya utawala bora na uraia kwa viongozi. Kupitia program hiyo viongozi 5,111 katika mitaa, vijiji, kata, na wilaya kwenye mikoa 17 wamejengewa uwezo wa kusimamia haki, kuwa wawajibikaji na kuzingatia usawa katika maeneo yao. Kati yao, wanawake walikuwa 1,550 (30.34%). Aidha, wananchi 9,906 nchi nzima waliweza kupata elimu ya uraia ambapo jumla ya wanawake 5,098 sawa na asilimia (51.48%) waliweza kunufaika.

## Matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma za kisheria

Wizara, kwa kutambua umuhimu wa elimu katika kujenga jamii yenye misingi imara ya maadili, imetoa mafunzo ya utawala bora na uraia kwa Viongozi na Watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kupitia programu hiyo, jumla ya viongozi 5,111 kutoka katika ngazi za Mitaa, Vijiji, Kata, na Wilaya katika Mikoa 17 nchini wamejengewa uwezo wa kusimamia haki, kuimarisha uwajibikaji, na kuzingatia misingi ya usawa na haki katika utekelezaji wa majukumu yao. Kati ya viongozi hao, wanawake walikuwa 1,550 sawa na asilimia 30.34, jambo linaloonesha jitihada za kuimarisha ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi. Aidha, wananchi 9,906 nchini kote walipata elimu ya uraia ambapo kati yao wanawake walikuwa 5,098 sawa na asilimia 51.48. Hali hii inaonesha mwitikio mzuri wa wanawake katika kushiriki na kunufaika na elimu ya uraia, hatua inayochangia kuimarisha ushiriki wao katika masuala ya kijamii na maendeleo ya taifa.

Kupitia mifumo ya kidijitali ikiwemo Mfumo wa Haki Sheria na Kituo cha Huduma kwa Mteja kinachopatikana kwa kupiga simu namba 0262 160 360 au 0800 004 004, Wizara imefanikiwa kurahisha upatikanaji wa huduma za sheria kwa wananchi. Kupitia Kituo cha Huduma kwa Mteja wananchi wameweza kuwasilisha malalamiko ya kisheria, hoja mbalimbali, kufuatilia mwenendo wa mashauri, pamoja na kupata taarifa muhimu kwa haraka na kwa urahisi bila kulazimika kufika ofisini na kuonana na wataalam ana kwa ana.

Takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi cha kuanzia tarehe 14 Februari 2024 na 28 Februari 2026, Kituo cha Huduma kwa Mteja cha Wizara kimefanikiwa kutoa huduma kwa jumla ya wanawake 529. Kati



*Mawakili wa Serikali kutoka Wizara ya Katiba na Sheria wakiwasikiliza wananchi waliowasilisha changamoto zao kwa njia ya simu katika kituo cha huduma kwa mteja cha wizara ya Katiba na Sheria.*

ya mashauri waliyoyawasilisha, malalamiko 374 yamepatiwa ufumbuzi na kufungwa, sawa na asilimia 70.70% ya malalamiko yote yaliyopokelewa. Aidha Malalamiko 155, sawa na asilimia 29.30, bado yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji Matokeo haya yanaonesha jitihada za Wizara katika kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wakati, hususan kwa wanawake, kwa kutumia teknolojia kama nyenzo ya kuimarisha uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika utoaji wa huduma za kisheria.

## Hadithi za mafanikio ya huduma za kisheria zinavyowavusha wanawake kutoka kwenye changamoto za kisheria mpaka kwenye ushindi

Katika harakati za kutafuta haki, sauti za wanawake waliopata huduma za msaada wa kisheria katika maeneo mbalimbali nchini zinaelezea kwa undani safari yao kutoka kwenye changamoto mpaka kwenye ushindi. Kutana na Bi. Beata Augustine maarufu kama Bibi Queen mkazi wa Wilaya ya Moshi mkoa wa Kilimanjaro. Bi. Beata yeye alikosa fursa ya kumiliki ardhi kwa kigezo cha kuwa mwanamke. Kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia iliyofanyika mkoani Kilimanjaro mnamo tarehe 31 Januari, 2026 pande zote mbili zilikutanishwa na kujadiliana hatimaye Bi. Beata alipewa sehemu ya ardhi ambayo sasa anaimiliki kihalali.

"Nilinyanyaswa nikafukuzwa nyumbani nikaambiwa hakuna chako hapa nikaondoka nikaenda kuishi kwa Msamaria mwema, niliendelea kuteseka nikawa sijui hatma yangu nilipokutana na watu wa Msaada wa Kisheria wa Mama Samia nikawaelezea. Ndugu wakaitwa tukaongea ndipo nikapewa kipande cha ardhi nami sasa namiliki ardhi" alisema Beata.

Vedastine Magenda ni mkazi wa Mbezi katika Manispaa ya Ubungo jijini Dar es Salaam, Mama huyu alijikuta katika hali ngumu ya kukataa tamaa pale ambapo nyumba yake ilitangazwa kupigwa mnada na benki mojawapo hapa nchini kutokana na kushindwa kutekeleza masharti ya mkataba kwa kushindwa kufanya marejesho ya mkopo. Mama huyu alipoteza tumaini la kuendelea kuwa mmiliki halali. Huduma za Msaada wa kisheria zikasikika masikioni mwake.

"Kwakweli bila huduma hii ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia sasa hivi mimi na wanangu huenda tusingekuwa pamoja tena, maana tusingekuwa na pa kuishi tulipewa siku saba kuondoka kwenye nyumba yetu wenyewe na tusionekane lakini kweli haki ipo, bank wakaambiwa wasitusumbue tena tunaishi kwa amani na wanangu" alisema Magenda.

## Hitimisho

Mafanikio ya Wizara ya Katiba na Sheria katika kuwafikia wanawake toka kwenye changamoto za kisheria mpaka kwenye ushindi ni uthibitisho wa dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kujenga jamii yenye usawa kwa wote. Katika kauli mbiu ya Siku ya Mwanamke Duniani ya mwaka 2026 nchini Tanzania yenye kauli mbiu: "Haki na Usawa kwa Wanawake na Watoto wa Kike: Msingi Jumuishi Kuelekea Dira ya 2050" inadhihirisha kuwa ni wakati sasa wa kuangalia nyuma na kushangilia na hatuna budi kukaza mwendo zaidi kuelekea katika matamanio ya kila mwanamke na msichana kushiriki katika kuijenga Tanzania yenye uchumi na mapato ya juu ifikapo 2050.

Mafanikio haya yanatupa mwanga kuwa msingi huo jumuishi unaojikita katika haki na sheria ni jambo ambalo linawezekana.





# Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inavyosogeza huduma za kisheria zaidi na wananchi

**Na Leila Muhaji, Dodoma**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imetajwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Ibara ya 59 (1).

Jukumu kubwa la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kuishauri Serikali katika masuala yote ya kisheria ndani na nje ya nchi katika maeneo ya ushauri wa sheria, upekuzi na uchambuzi wa mikataba mbalimbali ya kiuwekezaji na uandishi na ufasiri wa sheria.

Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaiwakilisha serikali kitaifa, kikanda na kimataifa katika masuala yenye maslahi kwa taifa kama yalivyooneshwa katika Ibara ya 59 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na yanaainishwa katika Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268.

Miongoni mwa majukumu hayo ni kuishauri serikali kuhusu masuala yote ya kisheria ikiwamo mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania ni sehemu ya mkataba ama ina maslahi katika mikataba hiyo.

Aidha, kutoa ushauri kwa wizara, idara zinazojitegemea na taasisi za serikali kuhusu mchakato wa utungwaji wa sheria na masuala mengine yahusuyo sheria, na kutoa ushauri stahiki wa sheria zilizotungwa na Bunge, sheria ndogo na maazimio mbalimbali pamoja na kuandaa miswada ya sheria kwa ajili ya kuwasilishwa bungeni.

Majukumu mengine ni kuandaa hati zote za kisheria na maazimio kwa ajili ya kuidhinishwa na Bunge, kushauri na kudumisha uhusiano kati ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili kuleta ufanisi kuhusu suala lolote lililopo mahakamani na katika mabaraza.

Lingine ni kupokea taarifa kutoka kwa Wakili Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Mashtaka ili kushauri Serikali, Bunge na Mahakama.

Aidha, kuwasimamia maofisa sheria na mawakili wa serikali wote walioko katika wizara, idara na taasisi za serikali katika kutekeleza majukumu yao ya kisheria.

Katika kipindi chote na hususan katika Siku 100 za kipindi cha pili cha uongozi wa Awamu ya Sita wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi, kuhakikisha ofisi inakuwa daraja katika kuisaidia serikali katika eneo hili nyeti la kisheria.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari hivi karibuni akizungumza na vyombo vya habari, amebainisha namna Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inavyotekeleza kwa weledi na ubora majukumu hayo kikamilifu katika eneo nyeti la kuendesha kliniki za sheria katika mikoa mbalimbali nchini.

Akizungumzia huduma za kliniki ya sheria na mchango wake katika kutatua changamoto za wananchi hususan wa kipato cha kawaida na cha chini katika upatikanaji wa haki, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anasema ofisi ilibaini kuna changamoto kubwa kwa wananchi wa kawaida hasa walioko wilayani na mikoani katika kuzifikia huduma za kisheria.

Wananchi wamekuwa wakihangaika na hii ni kutokana na gharama za kupeleka mashauri mahakamani kuwa kubwa, na hivyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ikaona umuhimu wa kuwasogelea wananchi katika mikoa na wilaya zao.

"Kwa hiyo tulianzisha kamati za ushauri wa kisheria katika mikoa na wilaya. Baada ya kuanzisha tukaziwekea utaratibu au mwongozo wa kisheria wa mwaka 2024 unaolenga kuhakikisha tunasogeza huduma za kisheria hadi ngazi za wilaya na mikoa," anaeleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Anasema moja ya nyenzo za utekelezaji wa mwongozo huo ilikuwa kuanzisha kliniki za huduma za kisheria, hasa kamati za ushauri za kisheria zinapoundwa, inaenda sambamba na wiki nzima ya utoaji wa huduma za kisheria kupitia kliniki katika mkoa au wilaya ili kutoa huduma hizo bure.

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaendelea kubainisha kuwa, "Tofauti na utaratibu mwingine wowote, kliniki hizi za kisheria zinatoa huduma za kisheria kwa wananchi, mwananchi yule baada ya kuwasilisha shauri lake, lalamiko lake au jambo lake lolote linalohitaji msaada wa kisheria, tukishampa ule ushauri wa kisheria hauishii pale."

Anaongeza: "Tunaendelea naye kumfuatilia kwa sababu tunaweka rekodi kwamba shauri hili lilihusu nini, kama lilihusu ardhi basi tunaliweka katika rekodi zetu, na kutoa ushauri, na pia kuendelea kulifuatilia hata baada ya pale mpaka likafike mwisho na kuhakikisha kuwa suala hilo mwananchi limetatuliwa".

Lengo kubwa la kliniki hizi za kisheria ni kusogeza huduma za kisheria kwa wananchi katika ngazi ya mikoa na wilaya. Tayari mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma, Mwanza, Singida, Manyara, Simiyu na Dar es salaam imeshafikiwa na wananchi wamejitokeza kwa maelfu.

"…Lengo lilikuwa kusogeza huduma karibu na wananchi tukitimiza maono na matakwa ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa akisisitiza kusogeza huduma karibu na



*Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari akitoa hotuba ya Uzinduzi wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria bila malipo kwa wananchi wa mkoa wa Singida.*



*Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari akitoa Huduma ya Ushauri wa Kisheria kwa Mwananchi wakati wa Kliniki ya Sheria bila malipo mkoani Singida, kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego na kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Singida Mhe. Godwin Gondwe.*



*Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Samwel M. Maneno (kushoto) akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe, Albert Chalamila (kulia) Mwongozo wa uundwaji wa Kamati za Ushauri wa Kisheria za Mikoa na Wilaya, wakati wa uzinduzi wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria ya Mkoa wa Dar es Salaam.*

wananchi, na kuwapa huduma kutoka kwa mawakili wabobezi.

"Lengo la pili ni kuwapunguzia gharama wananchi. Ameongeza kuwa, "Huduma hizi tunazitoa bure, kwa hiyo mwananchi anakuja anapata huduma na anaondoka. Kwa hiyo gharama zile tunawaondolea kwa sababu wanakuja kupata huduma," anaeleza Mheshimiwa Johari.

Katika kuhakikisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inapanua wigo zaidi wa utoaji wa huduma za ushauri wa kisheria bila malipo kwa wananchi, hivi karibuni Uzinduzi wa Kamati za Ushauri wa Kisheria na Kliniki za Kisheria zilizinduliwa katika mikoa ya Singida, Manyara na Simiyu ambako wananchi zaidi ya 5,800 walipatiwa elimu ya sheria na kutatuliwa migogoro yao.

Anazitaja kero kubwa zilizojitokeza ni ardhi ambayo imebeba malalamiko 66.

"Ardhi ni eneo ambalo kama serikali inabidi tuweze kuliangalia vizuri kwa kushauriana na wizara na wadau wengine katika masuala ya ardhi ili kuona tunapunguzaje migogoro hiyo ya ardhi," anaeleza Mheshimiwa Johari.

Mengine yaliyolalamikiwa ni mirathi, ndoa na madai. Anabainisha kuwa kwa kushirikiana na wadau kuna umuhimu mkubwa wa kuja na mbinu za kupunguza kero hizo zikiwamo sheria na sera kwa kushirikiana.

Hivi karibuni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam imezindua Kamati za Ushauri wa Kisheria na Kliniki ya Sheria bila malipo kwa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam ambayo ilifanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, ambako kazi hii iliendeshwa kwa nia ya kutoa elimu ya kisheria na kutatua changamoto za kisheria kwa wananchi na kuzipatia ufumbuzi wa kudumu.

Akizungumzia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 hasa eneo la kisheria, Mheshimiwa Johari anasema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeshiriki kikamilifu katika utekelezaji wa maandalizi ya dira hiyo mpya na hata ile inayomalizika mwaka huu.

Anasema, "Na pale itakapokuwa imepitishwa sasa na kuanza kutumika, basi na sisi tunaanza utekelezaji wa kuhakikisha kwamba kule tunakotaka kufika mwaka 2050, tunaweza kufika huko".

Anaongeza: "Kwa sababu kwenye dira tunazungumza kwamba tunataka kuwa na taifa ambalo litakuwa limepunguza umaskini kwa kiasi kikubwa na kuhakikisha uchumi wetu unakuwa na kufikia ngazi ya uchumi wa kati wa juu".

"Sasa lengo hilo ni kubwa, lakini tunaweza tu kufanikiwa kulifikia kama tu tutahakikisha kila mdau na kila mshiriki wa maendeleo na uchumi anachukua nafasi yake stahiki na kufanya yale ambayo yanapaswa kuhakikisha sisi tunafika huko tunakotarajia kufika mwaka 2050," anafafanua Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Anaeleza kwamba kwa kuwa dhamira ni kubwa hana wasiwasi kuwa nchi itaweza kufika huko, na hivyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imejipanga kuhakikisha yale yote yanayoihusu ili kufika huko 2050, yanafanyika ipasavyo.

"Baada ya kuisoma dira ile kwa kina na kuielewa jambo la kwanza ambalo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tunatakiwa kuhakikisha tunalitekeleza ni kuhakikisha tunaoanisha vizuri sheria tulizonazo na kule tunakotaka kwenda," anaeleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Anaongeza: "Ili kufika tunakotaka kwenda, lazima kuwa na 'legal framework' (mpango wa kisheria) kutuwezesha kufika kule. Yaani sheria ni kama daraja la kutuvusha upande huu wa 2025 na kutufikisha 2050 upande ule, hivyo ni lazima tuwe na hilo daraja."

Anasema kwa msingi huo, sheria zote lazima zioane. "Tusipofanya hivyo, tutakuwa tunakwenda 2050, lakini sheria zinavuta nyuma."

"Ndio maana tunafanya marekebisho ya sheria; lengo ni hilo ni ili kunyumbulika na jamii inavyokwenda, unanyumbulika na sekta za kiuchumi zinavyokwenda, unanyumbulika na changamoto mbalimbali zinavyokwenda. Kwa hiyo katika dira hii zimedadavuliwa vizuri na jinsi zitakavyokwenda ili kufika 2050," anaeleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

# Wafungwa zaidi ya 400 watunukiwa vyeti baada ya kuhitimu mafunzo wakiwa gerezani



*Wa kwanza kulia ni aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, akimkabidhi mfungwa cheti cha ujasiriamali baada ya kuhitimu mafunzo kwa njia ya mtandao Agosti 6, 2025 gereza kuu Arusha, mafunzo yaliyoandaliwa na Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na chuo cha Uhasibu Arusha ( IAA )*

Jeshi la Magereza Tanzania lina jukumu la kuwapokea, kuwahifadhi na kuwarekebisha wale wote ambao huletwa gerezani kwa mujibu wa sheria kupitia programu mbalimbali za stadi za kazi, ili wakitoka gerezani waweze kujitegemea huku wakiwa raia wema.

Mnamo, Machi 11, 2025 ilizinduliwa Programu maalumu ya Urasimishaji wa ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo yaani, (Recognition of Prior Learning - RPL), na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Innocent Bashungwa, ambao ulisaidia Jeshi kuingia mikataba ya ushirikiano na baadhi ya taasisi za elimu, ikiwemo Taasisi ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) pamoja na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), hali iliyowezesha wafungwa zaidi ya 400 kutunukiwa vyeti.

Programu ya kuwapatia vyeti wafungwa ni hatua muhimu kwa jeshi katika dhana ya urekebishaji kwani inatoa hamasa kwao ya kujifunza na kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za urekebishaji ili kupata ujuzi, elimu, maarifa na kuwawezesha kutambuliwa na jamii kwa ajili ya kuwasaidia kujiajiri au kuajiriwa pindi watakaporudi katika jamii baada ya kutumikia vifungo vyao magerezani.

Vyeti hivyo vilitolewa katika awamu, mikoa na fani mbalimbali ikiwemo umeme, ujenzi, ufundi rangi, bomba, magari, upishi, ushonaji na seremala, ambapo awamu ya kwanza ilikuwa ni vyeti vilivyo tolewa na VETA kwa Wafungwa 201 mkoani Morogoro, na wengine 73 walitunukiwa vyeti kama hivyo mkoani Mbeya na Wafungwa 170 mkoani Arusha, ambao walihitimu mafunzo ya Ujasiriamali na Stadi za Biashara, huku pia Wafungwa wengine 372 wameshatambuliwa ujuzi wao na Magereza ambapo hivi karibuni watafanyiwa udahili na kupatiwa vyeti na VETA.

Aidha, ili kuendelea kutoa mafunzo bora kwa wafungwa, Jeshi la Magereza limefanikiwa kuandaa mitaala mipya ikiwa ni hatua za kuboresha utoaji wa mafunzo stahiki kwa watumishi, lakini pia umeandaliwa muongozo wa programu za urekebishaji ambao umeweka misingi thabiti na utaratibu wa mapokezi, tathmini ya urekebishaji na kuwaandaa wafungwa kurejea kwenye jamii wakiwa raia wema.

Mitaala hiyo imeandaliwa kwa kushirikiana na Chuo cha Ustawi wa Jamii, Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW).

Pamoja na utoaji vyeti kwa wafungwa, jeshi pia limetanua wigo wa huduma ya usafirishaji na usindikizaji wa mahabusu kwenda na kurudi kutoka mahakamani, ambapo hivi karibuni mkoa wa Mbeya umeongezwa katika utoaji wa huduma hiyo, huku likishirikiana na Mhimili wa Mahakama kuwezesha usikilizwaji wa mashauri ya rufani kwa wafungwa kwa ngazi ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani, kwa njia ya Mahakama Mtandao.

Jeshi la Magereza linashirikiana na taasisi mbalimbali katika utunzaji wa mazingira, baadhi ya taasisi zinazoshirikiana na Jeshi la Magereza ni Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF), na TFS katika ufugaji wa nyuki na kupanda miti katika maeneo ya magereza yote nchi nzima ambapo katika kipindi cha mwaka 2024 hadi Januari 2026 Jeshi la Magereza limepanda miti Milioni 2.7, huku malengo kwa mwaka 2026 yakiwa ni kupanda miti Milioni mbili.

Pia jeshi limefanikiwa kuachana na matumizi ya kuni na kuhamia kwenye nishati safi katika kupika chakula cha wafungwa magerezani, ununuzi wa mashine za kutengeneza mkaa mbadala huku watumishi wa jeshi zaidi ya 15,000 wakinufaika na mpango wa matumizi ya nishati safi kwa kupatiwa mitungi na majiko ya gesi.

Aidha, katika kulinda mipaka, jeshi linaendelea na zoezi la upimaji wa ardhi na kupata hati miliki, ukarabati wa miundombinu ikiwemo ya magereza makubwa ya Keko na Ukonga, ujenzi wa magereza katika wilaya 12 ambazo hazikuwa na huduma ya magereza, ujenzi wa nyumba za makazi ya watumishi, ujenzi wa viwanja vipya vya gwaride Makao Makuu ya Magereza Dodoma na Chuo KPF Morogoro, ujenzi wa ukumbi wa mikutano na sherehe (Rugimbana Hall) ulioko eneo la Msalato jijini Dodoma ukiwa na uwezo wa kuchukua watu zaidi ya 500, kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalamu wa fani mbalimbali pamoja na kilimo cha umwagiliaji.

Yote haya hufanyika ikiwa ni kutimiza majukumu ya msingi ya jeshi ambayo mojawapo ni kurekebisha tabia za wafungwa lakini pia ni kutekeleza maagizo ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyoyatoa Machi 25, 2022 alipotembelea kwa mara ya kwanza Makao Makuu ya Magereza, na kulitaka jeshi lijikite katika urekebishaji wa wafungwa, bila kusahau maagizo ya Tume ya Haki Jinai iliyoundwa na Mhe. Rais ambayo nayo ilisisitiza Jeshi la Magereza kufanya zaidi shughuli za urekebishaji.

Pamoja na jitihada hizi za kuwapa ujuzi wafungwa na kuwafanya kuwa raia wema, Jeshi la Magereza linatoa wito kwa jamii kushiriki kikamilifu katika kuwarekebisha wafungwa kwani suala la urekebishaji ni mtambuka si la magereza pekee.









# TFC inavyojivunia usambazaji wa mbolea kwa wakati

*KUSHOTO: Mkurugenzi Mkuu wa TFC, Bw. Samuel Mshote akitoa ufafanuzi wa ubora wa mbolea za TFC.*
*KULIA: Tumbaku iliyostawi inayotumia mbolea ya Nitrogen Phosphorus Potassium (NPK).*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Mbolea Tanzania (TFC) ni Taasisi ya Serikali iliyopo chini ya Wizara ya Kilimo, iliyoanzishwa mwaka 1968 chini ya Sheria ya Makampuni (Companies Ordinance CAP 212), inayotambuliwa kwa sasa kama Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 (Companies Act, CAP 212),

## Dira

Dira ya TFC ni kuwa Kampuni inayoongoza na kutegemewa katika Uagizaji, Uzalishaji na Usambazaji wa Mbolea na Pembejeo nyingine za kilimo kuendana na mazao na mahitaji ya udongo na mazao Nchini.

Dira hiyo inalenga kuanzisha na kuendeleza viwanda vya ndani vya mbolea, kupunguza utegemezi wa mbolea zinazoagizwa nje, kuongeza ajira na tija katika Sekta ya Kilimo pamoja na kuhakikisha wakulima wanapata Mbolea Bora kwa wakati na kwa bei nafuu

## Dhima

Kutoa suluhisho sahihi la rutuba ya udongo na mahitaji ya virutubisho vya mazao kwa wakulima ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla.

## Mchango wa TFC

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TFC, Bw. Samuel Mshote kwa Habari LEO hivi karibuni, inaeleza kuwa chini ya Uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake ya kimkakati ili kuhakikisha upatikanaji wa Mbolea Bora Nchini.

Anasema, ndani ya siku 100 za Uongozi wa Rais Samia, TFC imesambaza jumla ya tani 140,500 za mbolea kwa wakulima katika maeneo mbalimbali ya Nchi. Mbolea hizo ni pamoja na DAP tani 49,500 kwa ajili ya kupandia mazao, UREA tani 11,000 kukuzia, CAN 27% - tani 10,000 kwa ajili ya kuongeza virutubisho katika mimea baada ya kupanda mazao, NPK tani 70,000 kwa ajili ya mazao ya tumbaku.

Anafafanua kuwa, hatua hiyo imeimarisha upatikanaji wa pembejeo kabla ya misimu ya kilimo, kuongeza uzalishaji wa mazao, na kuimarisha usalama wa chakula nchini, na kwamba mafanikio hayo yanaakisi dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuifanya sekta ya kilimo kuwa kichocheo cha uchumi wa Taifa.

## Miradi ya kimkakati

Katika kuimarisha uzalishaji wa ndani na kupunguza utegemezi wa uagizaji mbolea, kipindi hiki cha siku 100 za Rais, Daktari Samia Suluhu Hassan, TFC inaendelea kutekeleza miradi kadhaa ikiwemo, kukamilisha usimikaji wa mitambo ya kuchanganya mbolea (Bulk Bleeding Facilities) yenye uwezo wa kuchanganya tani 120 kwa saa, kinachojengwa Kurasini.

Aidha, TFC inaendelea na uimarishaji wa upatikanaji na uhifadhi wa mbolea, ili kuwepo kwa mbolea kwa wakati wote wa msimu wa kilimo kwa kukarabati ghala la Mwanza, Makambako na Sumbawanga. Bw. Mshote anasema Miradi hii inalenga kuongeza uwezo wa uzalishaji, uhifadhi na usambazaji wa mbolea nchini.

## Ushirikiano wa kitaasisi

Katika kutekeleza majukumu yake, TFC inaratibiwa na Wizara ya Kilimo, pamoja na TFRA (Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania), pia inashirikiana TARI (Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania), na TPHPA (Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania), ushirikiano ambao umeimarisha Udhibiti wa Ubora, katika usambazaji wa mbolea na ufanisi kutokana na afya ya udongo.

## Maeneo ya huduma

Mshote anasema katika kipindi cha siku 100 za Rais Samia madarakani, vituo vya kuhifadhia mbolea, vimeongezeka kutoka 20 hadi 22, vituo hivyo ni Dar es Salaam, Karatu, Arusha, Moshi, Morogoro, Tabora, Shinyanga, Kasulu, Mpanda, Sumbawanga, Makambako, Mbeya, Iringa, Tunduru, Songea, Mwanza, Geita, Tarime, Dodoma, Babati, Namtumbo, na Songwe.

## Mafanikio ya TFC

Mkurugenzi huyo amesema kuwa kuimarika kwa upatikanaji wa mbolea bora na kwa bei nafuu kwa wakulima ni miongoni mwa mafanikio makubwa ya TFC, sambamba na ongezeko la uzalishaji na ubora wa mazao ya chakula na biashara.

Aidha, TFC ilisambaza tani 140,500 za mbolea katika maeneo mbalimbali ya nchi, zikiwemo tani 49,500 za DAP kwa kupandia, tani 11,000 za UREA kwa kukuzia, tani 10,000 za CAN kwa kuongeza virutubisho baada ya kupanda, na tani 70,000 za NPK maalum kwa zao la tumbaku, Kwa TFC kusambaza tani 140,500 kumewezesha wakulima kupata pembejeo mbolea kabla ya kuanza shughuli za uzalishaji wa mazao hali ambayo itamuwezesha mkulima kuzalisha kwa tija na kuwa na utoshelevu wa mazao ya chakula na biashara kama sera ya nchi inavyoeleza.

Pia kuanzishwa kwa mfumo wa kidijitali wa ufuatiliaji wa mauzo ya mbolea kumewezesha udhibiti wa upotevu wa mbolea.


Ameongeza kwa kusema, uwekezaji katika mtambo wa kuchanganya mbolea wenye uwezo wa kuchanganya tani 120 kwa saa unaotarajiwa kuwekwa kurasini, Dar es Salaam ni mafanikio mengine ya kujivunia kwa TFC

## Wito kwa wakulima

Katika kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita za kuifanya sekta ya kilimo kuwa kichocheo cha uchumi wa taifa, TFC inatoa wito kwa wakulima wote kutumia mbolea bora, zilizothibitishwa na Wataalam.

TFC inasisitiza umuhimu wa wakulima kuzingatia ushauri wa wataalamu wa kilimo kuhusu aina na kiwango sahihi cha mbolea kulingana na mahitaji ya udongo na zao husika. Aidha, inawahimiza wakulima kununua pembejeo kupitia vituo rasmi na mawakala waliothibitishwa ili kuhakikisha wanapata bidhaa zenye ubora unaokidhi viwango vya kitaifa na kuepuka bidhaa bandia.









*JUU: Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Paul Makonda (Wapili kushoto), akiwa pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ambaye pia ni Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa (Wapili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Bi. Asha Dachi (kushoto), wakiongozana na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, wakati wa ziara maalum ya ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa Mradi wa Kiwanda cha Kisasa cha Uchapaji katika Makao Makuu ya TSN, Jijini Dar es Salaam, tarehe 15 Machi 2026.*

*CHINI KUSHOTO: Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) Bi. Asha Dachi akiwa katika kikao cha kazi na sehemu ya viongozi wa TSN.*

*CHINI KULIA: Moja ya mitambo ya uchapaji TSN.*

# Serikali ilivyoiwezesha TSN kufanikisha mageuzi makubwa ndani ya siku 100

KATIKA kipindi cha siku 100 tangu aapishwe kuingia madarakani Novemba 3, 2025, kufuatia Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 29, 2025, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kuonesha dira thabiti ya uongozi unaozingatia uwajibikaji, uadilifu na maendeleo endelevu ya taasisi za umma, sambamba na kuboresha ustawi wa watumishi wa umma.

Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), ambayo ni taasisi ya umma iliyo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ni miongoni mwa taasisi zilizonufaika moja kwa moja na sera, miongozo na mipango iliyotekelezwa na Serikali katika kipindi hiki.

TSN ina dhamana ya kuandaa, kuchapisha, kusambaza na kuendeleza magazeti ya Serikali, ya Daily News na HabariLEO pamoja na Majukwaa ya Kidigitali. Kupitia mamlaka yake, TSN ina jukumu la kutoa taarifa sahihi, za kuaminika na kwa wakati kuhusu sera, mipango, mafanikio utekelezaji wa miradi ya kimkakati na shughuli mbalimbali za Serikali, pamoja na kukuza maadili, uzalendo na mshikamano wa kitaifa kupitia vyombo vyake vya habari. Katika kipindi cha siku 100 TSN inajivunia yafuatayo:

## Uimarishaji wa Rasilimali Watu na Kuongeza Ufanisi wa Utendaji

Serikali katika kipindi hiki cha siku 100 imewezesha utekelezaji wa sera za

kuimarisha rasilimali watu katika Taasisi, ikiwemo utoaji wa ajira kwa jumla ya watumishi 74 wa kada mbalimbali. Hatua hii imeongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi wa Taasisi na kuimarisha uwezo wa kiutumishi wa TSN katika kutekeleza majukumu yake kwa weledi unaotarajiwa.

Ajira hizo zimeelekezwa katika maeneo ya kimkakati, yakiwemo Kurugenzi ya Huduma za Taasisi, Kurugenzi ya Habari, Kitengo cha Huduma za Uchapaji, Kitengo cha Ununuzi, Kurugenzi ya Uendelezaji Biashara, Kitengo cha TEHAMA na Takwimu, Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu za Ndani, pamoja na Kitengo cha Uhusiano kwa Umma na Nyaraka. Mgawanyo huu umezingatia mahitaji halisi ya kiutendaji, kudumisha uthabiti katika kuhabarisha umma, uzalishaji, usimamizi na utoaji wa huduma.

## Uendelezaji wa Ujuzi na Uimarishaji wa Utaalamu

TSN imeendelea kutekeleza mpango endelevu wa mafunzo kwa watumishi wake, ambapo jumla ya watumishi 143 wamepatiwa mafunzo katika nyanja mbalimbali kulingana na majukumu yao. Mafunzo haya hayajalenga tu kuongeza ujuzi na maarifa ya kitaaluma, bali pia kuimarisha mshikamano, ushirikiano kati ya menejimenti na watumishi, pamoja na kukumbushana misingi ya maadili ya utumishi wa umma, uwajibikaji na taratibu za kazi.

Kupitia mpango huu, TSN imejenga msingi imara wa utendaji wenye weledi unaoendana na mabadiliko ya kiteknolojia na mahitaji ya sekta ya habari katika kuhudumia umma kwa ufanisi zaidi.

## Kuimarika kwa Ushirikiano wa Kimkakati wa Kimataifa

Serikali katika kipindi hiki pia imewezesha TSN kupanua na kuimarisha ushirikiano wa kimkakati na balozi na taasisi za nchi rafiki. Miongoni mwa ushirikiano huu ni kati ya TSN na Ubalozi wa China nchini Tanzania, Shirika la habari Xinhua, pamoja na Taasisi ya Viory ya Abu Dhabi, Falme za Kiarabu (UAE). Ushirikiano huu umefungua fursa za kubadilishana uzoefu, maarifa na teknolojia za kisasa katika sekta ya habari, uchapaji na usambazaji wa maudhui ya kidijitali.

Kupitia mahusiano haya, TSN imepanua wigo wa maarifa na mbinu bora za kimataifa, huku ikikidhi wajibu wake wa msingi wa kutoa habari zenye ubora na ushindani katika soko la ndani na nje ya nchi.

## Utekelezaji wa Mradi wa Ufungaji wa Mitambo ya Kisasa ya Uchapaji

Serikali imewezesha utekelezaji wa Mradi wa Ufungaji wa Mitambo ya Kisasa ya Uchapaji yenye teknolojia ya hali ya juu. Mitambo hii itarahisisha uchapaji wa magazeti ya Serikali kwa ubora na kasi, na pia kutoa huduma mbalimbali za uchapaji wa kibiashara ikiwemo vitabu, vipeperushi, mabango, nyaraka, vikombe, fulana (T-shirt) na bidhaa nyingine za matangazo.

Mradi huu unatarajiwa kuongeza mapato ya ndani ya TSN, kupanua wigo wa huduma zake, kuimarisha ushindani katika sekta ya uchapaji, na kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa ujumla kupitia ajira na thamani ya uzalishaji wa ndani.


## Ujenzi wa Studio ya Kisasa na Kuimarika kwa Habari za Kidijitali

Vilevile, Serikali imewezesha ujenzi wa studio ya kisasa itakayohudumia shughuli za habari, mawasiliano na uzalishaji wa maudhui. Studio hii itatoa mazingira bora na ya kitaalamu kwa ajili ya utayarishaji wa vipindi, mahojiano na maudhui mengine ya kimtandaoni. Sambamba na hilo, upatikanaji wa vitendea kazi muhimu ikiwemo kompyuta na vifaa vya TEHAMA umeongeza ufanisi, kasi na ubora wa utendaji.

Aidha, Serikali imewezesha maboresho ya gazeti la mtandao la TANePress, hatua inayopanua wigo wa usambazaji wa habari na taarifa za Serikali ndani na nje ya nchi, kwa haraka, kwa usahihi na kufikia wananchi wengi zaidi, ikizingatia viwango vya taaluma ya habari katika zama za kidijitali.

Kwa ujumla, mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha siku 100 yanaonesha kwa uwazi dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuimarisha taasisi za umma, kuendeleza uwajibikaji na kuchochea maendeleo endelevu yenye tija kwa Taifa. Hatua hizi zimeweka msingi imara wa mageuzi ya kiutendaji na kimkakati ndani ya taasisi za Serikali, zikiwemo sekta ya habari.

Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) inatoa shukrani za dhati kwa Serikali kwa uongozi wake mahiri, maono mapana na msukumo thabiti katika kuimarisha taasisi na kuboresha mazingira ya utendaji. TSN inaendelea kuahidi kushirikiana kwa karibu katika kutekeleza majukumu yake kwa weledi, uadilifu na uzalendo, huku ikiendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na kumtakia mafanikio tele katika safari yake ya kuwatumikia Watanzania wote.





# KATALOGI YA BIASHARA

TANZANIA STANDARD NEWSPAPER

"Kampuni ya Magazeti ya Serikali"

## Bidhaa na Huduma Zetu

- **Magazeti** na Majarida
- **Uchapishaji** wa Kibiashara
- **TANePress Gazeti** la Mtandaoni
- **Ushauri wa Vyombo** vya Habari
- **Matangazo**
- **Jukwaa la** Biashara
- **Huduma Maalum** za Vyombo vya Habari
- **Maktaba ya Kidigitali** na Upigaji Picha wa Kibiashara

## KWA NINI UTUCHAGUE SISI?

1. Chombo cha habari cha Serikali.
2. Uzoefu wa miaka 90.
3. Huduma zisizo na usumbufu na uwasilishaji kwa wakati.

**Mkurugenzi Mtendaji: 0786 467 133**
**Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara: 0765 288 798**
**Meneja wa Mauzo na Usambazaji: 0653 912 475**
**Meneja wa Masoko na Utangazaji wa Bidhaa: 0754 492 310**
**Meneja wa Kitengo cha Uchapaji: 0745 599 029**

***Sisi ni Magwiji wa Uchapishaji.***





# HABARIKA NASI SASA




Habarika kupitia machapisho yetu **Habari leo** na **Daily news** kwa **Tsh. 1000/=**

Pamoja na **Spoti leo** Kidigitali kwa **Tsh. 500/=**

www.epaper.tsn.go.tz

habarileo_tz
dailynews_tz
Spotileo

HabariLeo
Dailynewstz
Spotileo

HabariLeo
Daily News Tanzania
Spotileo

Daily News Digital

# WADHAMINI



**Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba**
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



**Mhe. Hamza S. Johari**
Mwanasheria Mkuu wa Serikali



**Bw. Nehemiah Kyando Mchechu**
Msajili wa Hazina




**Mhe. Paul Christian Makonda**
Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo



**Mhe. Deogratius John Ndejembi**
Waziri wa Nishati



**Mhe. Abdallah Hamis Ulega**
Waziri wa Ujenzi



**Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo**
Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi



**Dkt. Juma Zuberi Homera**
Waziri wa Katiba na Sheria



**Jeremiah Yoram Katungu**
Kamishina Jenerali wa Magereza



**Bw. Masha J. Mshomba**
Mkurugenzi Mkuu wa NSSF



**Eng. Hassan Seif Saidy**
Mkurugenzi Mkuu wa REA



**Bw. Lazaro Twange**
Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO



**CPA(T) Mussa Makame**
Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC



**Eng. Charles Sangweni**
Mkurugenzi Mkuu wa PURA



**Dr. Baghayo Abdallah Saqware**
Kamishna wa Bima TIRA



**Eng. Victor H. Seff**
Mtendaji Mkuu wa TARURA



**Bw. Samuel A. Mshote**
Mkurugenzi Mkuu wa TFC

**MWEZESHAJI**



**Bi. Asha Dachi**
Mkurugenzi Mtendaji wa TSN

TANZANIA
STANDARD
NEWSPAPERS

**Jarida hili limeandaliwa na TSN**